

**KUJIFUNZA HABARI ZA
BIBLIA
(MWALIMU)**



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

Mwaka wa Kwanza

Kitabu cha Kwanza

KUJIFUNZA HABARI ZA YESU

VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

(MWALIMU)

Mwaka wa Kwanza

Kitabu cha Kwanza

Africa Coordinated Curriculum for Bible Study
J1-ITS

Used by permission of International Publications Services

Published and printed by
Baptist Publications House
Thika Road, Ruaraka
Box 30370, Nairobi

Soma Luka 18:22-23, na ujibu maswali juu ya mtu huyu.



"Mimi ndiye mtawala aliye-
kuja kwa Yesu.
Nilikuwa na
swali muhimu la
ku m w u l i z a .
Nilitaka kujua
kama ilinipasa
kufanya nini ili
nipate uzima wa
milele? Yesu
aliniambia niuze yote nilivyo navyo
na niwagawanyie maskini. Niliposikia
haya, nilihuzunika sana kwa sababu
nilikuwa tajiri sana.

"Bila shaka unanikumbuka! Nina
hadithi nzuri ya kusimulia. Kama
utasoma Luka 19:1-10 utapata kuona
ya kwamba mimi ni mtu gani, na
utaweza kujibu maswali haya.



"Jina langu ni Zakayo, na nilikaa
katika mji wa Yeriko. Yesu alipokuja
katika mji wetu, ilinibidi kupanda juu
ya mti ili niweze kumwona. Alikuja
karibu nami akanita kwa jina langu,
kisha akasema kwamba imempasa

kushinda nyumbani mwangu. Yesu
alibadilisha maisha yangu, nikawa
mwamini, nikataka kuhakikisha
upendo wake. Nilikuwa tayari kutoa
nyu ya mali yangu kwa maskini, na
kwa wale niliowang'anya kwa hila,
nawarudisha mara nne zaidi. Siku ile,
wokovu ulifika kwangu na kwa
nyumba yangu. Yesu alisema kwamba
alikuwa amekuja kutafuta na kuokoa
kile kilichopotea."

KULIFUNGA SOMO

Kila mojawapo ya hadithi hizi ina
ujumbe wenye uwezo kwetu sisi sote.
Inatupasa kumrufusu Kristo kutawala
maisha yetu bila kujali thamani
inaoitugharimu. Je, wanafunzi wako
wanekuwa na mawazo gani juu ya
mwito huu.

Labda utataka kuwapa wanafunzi
wako nafasi ya kuzungumza wakati
wa mwisho wa somo. Labda kuna
wavulana na wasichana darasani
mwako ambao hawajamweka Kristo
kwanza maishani mwao. Labda
hawajampokea Kristo kuwa Mwokozi
wao binafsi. Wakumbushe juu
yamaisha ya ajabu wanayoweza
kupata katika wokovu.

Unapofunga somo kwa maombi,
omba ili kwamba wewe pamoja na
kila mmoja wa wanafunzi wako
mtaweza kutambua mwito huo wa
kumweka Kristo kwanza katika
mambo yenu yote mnyofanya.
Omba ili kwamba uweze kujitoa
wewe binafsi kwa Yesu. Hivi ndivyo
tunavyopokea furaha halisi.

Katika vitabu vya waalimu kumeandikwa majibu ya maswali hayo. Jiweke tayari kuwapa wanafunzi wako majibu kamili. Lakini usiwe na tamaa ya kutoa majibu mara moja kwa kuwa ukifanya hivyo wanafunzi hawatafanya kazi yao. Wape wakati wa kutosha kufanya kazi yao wenyewe.

Kumbuka kwa somo hili ya kwamba kusudi letu ni la kuwasaidia wanafunzi wetu kutambua hitaji la kuwmeka Kristo kwanza maishani mwao.



"Yesu alikuja katika Ziwa la Galilaya ambako alikuwa mvuvi. Aliniambia nitweke mpaka kilindini, nikashusha nyavu zangu. Nilipofanya

hivyo, nilishika samaki wengi mno hata nyavu zangu zikaanza kukatika. Niliporudi tena ukingoni, Yesu alikuwa pale, na akasema ya kwamba atanifanya kuwa mvuvi wa watu. (SIMONI PETRO Luka 5:1-11).

"Soma Luka 5:10 na uwataje watu wengine wawili ambao walikuwa pamoja na Simoni, Yohana na Yakobo. Watu hawa waliacha vyombo vyao na vyote wakamfuata Yesu. (Luka 5:11)

WASAMARIA WENYE UKOMA

(Luka 17:14-16)

"Mimi pamoja na wenzangu wengine tisa tulimjia Yesu. Sisi sote tulikuwa wenye ukoma. Yesu alituhurumia siku hiyo. Alitumbua mkajionyeshe kwa Makuhani. Tulipofanya hivyo tulitakasika." Ni wangapi kati ya wagonjwa hawa walimshukuru Yesu? Mmoja tu! Je, alikuwa ametoka (wa kabila gani) wapi? Samaria.

Wakati mmoja, Bwana aliwachagua watu 70 kumtangulia kwenda katika vijiji na miji. Aliwatuma wawili wawili. Yesu aliwaambia kwamba mavuno yalikuwa mengi, lakini watenda kazi walikuwa wachache. Liliwapa kuomba ili Bwana wa mavuno apeleke watenda kazi wengi. Watu hawa waliambiwa wasichukue kitu cho chote. Basi waliondoka wakaenda katika miji na vijiji hivi. Na waliporudi, walisema, "Bwana, hata pepo wanatutii kwa jina lako."

(Watu waliotumwa kumtangulia Yesu Luka 10:1-2, 17)

Hadithi yangu inaanza katika Luka 15, kifungu cha 11 na 12. Soma vifungu hivi kwanza. Je, waikumbuka hadithi yangu na yale yaliyonipata? (Mwana Aliyepotea Luka 15:11-112, 18-24)

"Nilichukua fedha ambazo baba aliniwekea, nikaenda zangu nchi ya mbali. Na huko nilitumia fedha zangu zote, nikabaki bila cho chote, wala chakula. Nilikata shauri kurejea nyumbani (kifungu 18). Baba yangu alifurahi mno kuniona, hata akanipa joho na pete ya kutia kidoleni na viatu vya kuvaa kwa miguu. Nilikuwa nimepotea, na sasa nimeonekana."

VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA (MWALIMU)

Mwaka wa Kwanza

Kitabu cha Kwanza

YALIYOMO

Sura

Ukurasa

Ujumbe Kwa Mwalimu	4
1. Yesu Atembelea Miji Ziwani	5
2. Yesu Afanya Mijiza Ziwani	10
3. Yesu ni Tabibu Wa Ajabu	17
4. Yesu Afunua Utukufu Wake	22
5. Yesu Awatuma Wasaidizi Sabini	27
6. Yesu Aonyesha Ni Nani Jirani Mwema.	32
7. Yesu Azungumza Juu Ya Hazina Ya Mbinguni	37
8. Yesu Aeleza Juu Ya Kutafuta Kilichopotea	42
9. Yesu Asimulia Hadithi Juu Ya Watumwa Waaminifu	48
10. Yesu Afundisha Juu Ya Maombi	53
11. Yesu Aeleza Jinsi Ya Kumweka Kwanza Maishani	59
12. Yesu Amwoko Mtu Aliyekuwa Mtini	64
13. Somo La Marudio	69

SOMO LA MARUDIO

MASOMO YA BIBLIA: Luka 5:1-11; Luka 17:14-16; Luka 10:1-2, 4-17; Luka 15:11-12, 18-24; Luka 18:18, 22-23; Luka 19:1-10

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Masomo yaliyoandikwa katika kitabu hiki ni ya ajabu kujifunza. Tumekuwa na masomo kumi na mbili yenye hadithi tele juu ya maisha na kazi ya Bwana Yesu Kristo. Kwa kweli, masomo haya yametungoza sisi sote kujaribu kuishi kwa kujitoa kwa Kristo.

Kusudi letu katika masomo haya limekuwa ni kumweka Kristo kwanza maishani mwetu.

Labda sasa ni wakati mzuri wa kurudia masomo yote ya kitabu hiki ili tuone vile lengo hilo limeimiza.

Je, wanafunzi wako wamekuwa na mawazo gani juu ya masomo haya? Wamefanya juhudi ya kujaribu kufuata milano ya wanaume na wanawake hawa ambao tumekwisha kujifunza juu yao? Je, waona badiliko lo lote katika lamaa yao ya kumweka Kristo kwanza katika maisha yao? Umekwisha kupokeaje mafundisho kutoka masomo haya?

Haya yote ni maswali ambayo wewe kama mwalimu yataa uyajibu. Kwa kuyajibu, kama mwalimu yataa uyajibu. Kwa kuyajibu, waweza kuona vile umekwisha kuwasaidia wanafunzi wako vyema, na pia kuona mahitaji waliyo nayo. Somo la leo labda

litakuwa lenye msada kwako katika kuyarudia mafundisho na mifano ambayo wanafunzi wako wamekwisha kusikia wakati wa mafunzo.

Unahitaji kusoma Maandiko na kujua hadithi hizo barabara. Labda wanafunzi wako wataona kwamba wana maswali muhimu ya kuuliza wakati wanapojaribu kukumbuka hadithi hizo. Utahitaji kuwa tayari kuwapa majibu wanayotaka. Labda utependa kujitayarisha wewe mwenyewe pia kwa njia ya maombi. Omba ili kwamba uweze kuwasaidia wanafunzi wako kutambua hitaji la kumweka Kristo kwanza maishani mwao.

Somo hili la marudio la leo limeandikwa katika njia tofauti na masomo mengine ambayo tumekwisha kujifunza. Ulapata hadithi sita mbalimbali zikwa na nafasi za kujaza na maswali ya kujibu. Ulaata wanafunzi wako wasome kwanza Maandiko. Maandiko haya yatasimulia hadithi za watu fulani ambao tumekwisha kujifunza katika masomo yaliyopita.

Wewe kama mwalimu, labda utapenda kuwaongoza wanafunzi wako katika mazungumzo juu ya kila hadithi ili kuwakumbusha wanafunzi wako juu ya somo ambalo Yesu alifundisha wakati alitupa milano hii. Kwa kufuata mazungumzo haya, utahitaji kuwasaidia wanafunzi wako kujibu kila swali juu ya watu hawa.

Una nafasi nzuri wakati huu wa masomo haya kuwaambia wanafunzi wako habari za Yesu katika mfulizo wa hadithi zenye kupendeza. Baadhi ya masomo haya yatufundisha juu ya wokovu. Mengine yatufundisha juu ya maisha ya Kristo. Katika kila somo, jambo muhimu linalotiliwa mkazo ni "Yesu Kwanza." Mwana wa Mungu ni lazima "awe mtangulizi katika yote." (Wakolosai 1:18)

Kabla ya wanafunzi wako kutafuta majibu yake Mungu, wanahitaji kuuliza maswali ambayo yatawongoza kwa Neno lake. Ukiyatayarisha masomo vyema, waweza kuwaongoza wanafunzi wako kuyafikiria mambo anayoyasema Mungu juu ya maisha yao na matatizo yao.

Unapowaongoza wanafunzi wako katika mafunzo ya Biblia, uwaruhusuwasome Neno la Mungu.

K Zakayo alikuwa mtoza ushuru mwongo ambaye alichukiwa.

M Mti ambao Zakayo alipanda juu ulikuwa mtende.

K Yesu alimwambia Zakayo ya kwamba alitaka kuwa mgeni wake.

K Yesu aligeuza maisha ya Zakayo hata akawapa maskini mali aliyowanyang'anya kwa hila.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Uniondolee ubatili na uongo."
Mithali 30:8

Maandiko ya kifungu hicho yana maana zaidi ya maneno hivi hivi tu. Ni ombi lisemalo kwamba Bwana hataondoa tu majaribu ya dhambi hizi, bali ataondoa pia dhambi zenyewe. Hili ndilo ombi la Zakayo wakati alipopata furaha mpya ya kuwa mfuasi hasa wa Kristo. Labda ombi hili lafaa pia kuwa ombi la mmoja wa wanafunzi wako!

Mara kwa mara twajaribiwa kutenda dhambi kwa kusema uongo au kwa kutokuwa waaminifu. Pengine hakuna jaribu ambalo ni kuu zaidi ya hilo liwajialo wavulana na wasichana.

Wewe kama mwalimu, waweza kuwasaidia kuona kwamba wanaweza kuacha mambo hayo yasiyo mema kwa kumweka Kristo kwanza maishani mwao. Kwa kweli, tukimweka Kristo kwanza maisha yetu, anatupa uwezo wa kufanyika watu wapya. Na sehemu ya nafsi zetu za zamani ambazo twaweza kuziacha ndizo sehemu za kudanganya au kuiba.

KULIFUNGA SOMO

(Wape wanafunzi wako dakika chache za kunyamaza wakati huu wa kufungu somo. Wape wakati wafikirie juu ya mwito wa kumweka Kristo kwanza katika maisha yao na kuacha dhambi hizi nyuma.)

Unapofunga somo kwa maombi, labda utapenda kuwaruhusu baadhi ya wanafunzi wako kushiriki katika maombi haya. Usijaribu kuwalazimisha wanafunzi kuomba. Omba ili kwamba Mungu akusaidie wewe pamoja na wanafunzi hao wako kuwa na nia na furaha katika kumweka Kristo kwanza katika maisha yenu, na kwa kuishi maisha ya uaminifu.

YESU ATEMBELEA MIJI MIWILI

MASOMO YA BIBLIA: Luka
4:16-44

kusoma unabii huu kama unavyopatikana katika Isaya 61:1-2.

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Somo hili ndilo somo la kwanza kati ya masomo yaitwayo "Kujifunza Habari za Yesu." Somo hili ni chanzo cha kichwa ambacho tutakiita, "Yesu kwanza." Mikazo ya masomo haya ni karibu sawa. Yaani, Mungu ataka tutoe kabisa maisha yetu kwake. Kila somo litakaza njia fulani ambayo twaweza kujitoe kwa uongozi wake Mungu.

Ni Yesu tu aliyekuwa mtu wa pekee mwenye maisha kamili maisha yasiyo na dhambi. Tukitaka kuishi kama Kristo ni lazima tufuate mfano wake. Si rahisi kwetu kila siku kufanya mambo ambayo yanaweza kuonyesha kwamba Kristo ndiye wa kwanza maishani mwetu. Kuishi maisha ya Kikristo kunahitaji uangalifu siku zote. Twahitaji kukumbushwa njia ambazo twaweza kufuata mfano wa Kristo.

Mafundisho yetu juu ya maisha ya Yesu na kazi yake yanaanzia Nazareti, mjini kwao alikozaliwa. Ni katika Mji huu ambako Yesu alifukuzwa kwa sababu watu hawakuamini kwamba ba esu alifukuzwa kwa sababu watu hawakuamini kwamba alikuwa kweli Mwana wa Mungu. Watu hawa wa Nazareti walikuwa Wayahudi na walijua unabii wa Isaya. Utahitaji

Wewe kama mwalimu una nafasi ya kuwasaidia wanafunzi wako kuamini ahadi ya Yesu. Lakini waweza kuwaongoza kuamini kwamba Kristo ndiye wa kwanza ikiwa wewe waamini ahadi hiyo. Je, unampa Kristo nafasi ya kwanza maishani mwako?

Unapojitayarisha kufundisha, kumbuka mwenyewe kuwa unahitaji kufanya uwezekano wa kumruhusu Kristo kuwa wa kwanza katika maisha yako kila siku. Ufundishapo, kusudi yako lafaa kuwa la kuwaongoza wanafunzi wako kuelewa kuwa wanapaswa kukata shauri kumkataa au kumwamini Kristo kuwa Mwokozi wao. Wasaidie wanafunzi wako kuona kwamba kwa kumwamini Kristo tunafanya ahadi ya kumpa nafasi ya kwanza maishani mwetu. Yatupasa kuendelea kufanya wajibu huu wetu ili kutimiza ahadi hiyo.

MAMBO YA KUKAZA

1. Yesu hakufanya miujiza Nazareti kwa sababu watu hawakumwamini, tena walimkataa.
2. Yesu alifanya miujiza Kapernaumu kwa sababu watu wa mji huo walimpokea.
3. Je, tumeshampokea Yesu maishani mwetu?

KULIFUNDISHA SOMO:


Sema: Kwa mfano, mvulana au msichana wa rika lako amekuja shuleini mwako. Utawezaje kumfahamu? Ni jinsi gani utakata shauri kama wataka yeye awe rafiki yako maalum?

Wakati mwingine, rafiki mgeni huwa na mambo mazuri yenye kustajabisha kuwaambia kuhusu mahali ambapo amekuwa akikaa, au kutembelea, au kuwaambia jambo ambalo limekwisha kumfanyikia. Mara kwa mara, hadithi hizi zake tunaweza kuzidhamia kuwa si zakuuminika. Hata tunaweza kuwa na shaka, nakujiliza kama anatumbea ukweli au anatumdanganya.

Yesu alipokuwa hapa ulimwenguini alizunguka huku na huko akiwaambia watu habari zake. Watu walionsikia walilazimika kukata shauri kuamini maneno aliyokuwa akayasema kuwa ni ya kweeli, au kumkataa.

Sema: Hebu twende kwa miji miwili ambayo Yesu alitembelea na kuona jinsi watu wengi walivyomtenda.

Yesu alirudi kijijini Nazareti. Ni katika mji huu ambapo alifanya kazi na Yusuftu, baba yake mtezi, ambaye alikuwa seremala. Na hapa ndipo alitumika miaka yote ya ujana wake. Na sasa alitaka kuwaambia watu habari ya kwamba yeye ndiye Mashihi aliyehidiwa, na ambaye walimtumainia kuja kwa muda wa miaka mingi. Kwanza alikwenda sinagogi. (Mwambie mwanafunzi mmoja asome Luka 4:16.)



Uliza: Je, wajua kuwa sinagogi ni nini? (Ngojia upate jibu.) Sinagogi ni jengo ambamo Wayahudi humwabadu Mungu.

Yesu alipoingia ndani ya sinagogi, aliondoka na watu kusoma Maandiko. Watu hao hawakuwa na Biblia kama hivi tunavyo siku hizi. Yesu alisoma Maandiko kutoka hati ya kuviringisha. Hati hizi zilikuinjuliwa wakati wa kusoma. Mkuu wa sinagogi alimpa Yesu hati

nayo. Alihuzunika juu ya uongo na unyang'anyi wake baada ya Yesu kuigeuza roho yake. Lakini je, kuhuzunika tu kwamba ametenda dhambi kuliosha? La. Ilimpasa kuonesha kwamba alikusudia kurudisha vitu au fedha alizonyang'anya na kwamba hataita tena.

Hebu sasa tuiangalie sisi wenyewe. Je, utakuwa mtu wa namna gani unapoishi kwa kufuata njia zako mwenyewe? Je, u mchoyo? Je, unemdanganya mwingine au unemwibia mwingine? Je, umepata kuwaambia wazazi wako au mwalimu wako uongo? Ukitaka kumweka Kristo kwanza maishani mwako utahitaji kufanya nini? Ndiyo, ni lazima umbe msamaha. Kisha ni lazima urekebisha mambo uliyowakosea wengine.

Mwala yule tajiri aliposikia thamani ya kumweka Kristo kwanza maishani mwake, aliondoka akaenda zake. Hakukusudia kutoa thamani hiyo. Lakini Zakayo alikuwa na nia, na kwa furaha alilipa thamani ya dhambi na hatia yake. Je, wakusudia kuweka Kristo kwanza maishani mwako na kuacha kutotii?

KAZI YA KUFANYA

Kata neno lisilo sawa katika sentensi zifuatazo, kisha andika neno lililo sawa katika mstari ulio kando ya kila sentensi.

tajiri Zakayo, mkubwa wa watoza ushuru, alikuwa ~~maskini~~

Zakayo ~~yonetani~~ alitaka kumwona Yesu, lakini hakuweza kwa sababu ya umati wa watu.

mfiupi Zakayo alikuwa mtu ~~mtete~~ mti. Alitambua mbele ya umati akapanda juu ya ~~mwamba~~

Maisha ya Zakayo yaligeuka kuwa mema wakati ule alipokutana na Yesu. Twajuaje ya kwamba jambo hili ni kweeli? Andika neno "Ndiyo" kando ya sentensi ambayo ni kweeli.

Zakayo alisema kwamba alibadilika maisha.

ndiyo Zakayo alirudisha mara nne mali aliyowanyang'anya maskini kwa hila.

Yesu alisema kwamba alikuwa amekuja kufanya kazi maalumu. Andika alama hii (X) kando ya sentensi zenye sababu zilizomfanya Yesu kuja ulimwenguini.

Kutafuta na kuwaokoa watu wanaofikiri kwamba ni wema.

X Kutafuta na kuwaokoa watu waliopotea dhambi.

Kuwaifanya wenye dhambi kuburudika moyoni mwao.

Kama ungali kuwa katika umati ule siku ile ya furaha ungali mwona Zakayo pamoja na Yesu. Andika herufi "M" kando ya sentensi zenye makosa, na uandike herufi "K" kando ya sentensi ambazo ni kweeli.

K Zakayo alitangulia mbio mbele ya umati wa watu akapanda mti kumwona Yesu.

Biblia inatwambia kwamba, wakati ule ule mwujiza ulifanyika. Zakayo, mtu aliye kuwa mchoyo aligeuka kuwa mtu mpya. Alimpokea Yesu moyoni mwake, na wakati ule akawa mwana wa Mungu. Aligeuka kuwa mtu mwenye furaha zaidi; mwenye furaha kwa sababu alikutana na Yesu alishuka mtini, kisha yeye pamoja na Yesu wakaenda nyumbani kwake. Huko Yesu alikaa naye kwa sababu sasa alikuwa mwamini mpya.

Watu wa Yeriko hawakuwa na furaha. Hawakumtazamia Yesu kula pamoja na mwenye dhambi kama huyu. Walisahau kujua kwamba wao pia ni wenyewe dhambi, na kwamba Yesu alikuja kuwaokoa watu aliopotea katika dhambi. Na kusema kweli, majirani hawa hawakujua mwujiza ambao ulikuwa umegeuza roho ya Zakayo.

Ilimpasa Zakayo kufanya nini ili kuwaonyesha watu hawa ya kwamba aligeuza kiroho? Kwanza, kwa matendo yake aliwawezesha kujua kwamba sasa amekuwa mwamini mpya. Alimwita Yesu "Bwana" mbele ya jamaa, rafiki, na hata mbele ya maadui zake. Na kwa kumwita Yesu hivyo alikuwa akiwambia watu ya kwamba kutokea wakati ule Yesu ndiye atakayekuwa wa kwanza katika maisha yake. Alikuwa akimtaka Yesu kuyatawala maisha yake yote.

Hatimaye, ugeuzi mwingine mkuu zaidi ulifanyika tena maishani mwa Zakayo. Badala ya kuwanyang'anya watu hawa fedha zao kwa hila, alikusudia kuwapa maskini nusu ya mali yake. Sheria ya Musa iliamuru

mtu kutoa tu sehemu ya kumi ya mapato yake.

Badala ya kuchukua fedha nyingi kwa watu, Zakayo alisema kwamba atawarudishia mara nne watu aliowanyang'anya kwa hila.

Mtoza ushuru huyu alikuwa akitubu ya kwamba alikuwa amewatendea wengine ubaya. Alidhihirisha kwamba kulikuwa na ugeuzi ndani ya roho yake. Imani hasa katika Bwana Yesu kila wakati hujionyesha yenyewe katika kazi nzuri. Zakayo aliyarekebisha mambo kuwa sawa kwa sababu sasa alikuwa amekwisha kuzaliwa upya katika jamii yake Mungu. Alitaka kumweka Kristo kwanza katika maisha yake kwa kuepukana na hila na uongo.

Twajua kwamba Zakayo aligeuza kweli kwa maneno aliyosema na kufanya. Yesu alisema kwamba sababu iliyomfanya kutoka mbinguni kuja ulimwenguni ilikuwa ni kuwaokoa wenyewe dhambi. Vile Mwana wa Mungu alivyomtatua Zakayo na kumwokoa, ndiyo anavyokutafuta wewe leo ukiwa bado hujampokea kuwa Mwokozi wako.

Tumekwisha kuona nafasi kuu zilizomjia Zakayo maishani mwake.

Kabla ya kukutana na Yesu Zakayo alikuwa akiishi katika njia zake mwenyewe. Alitaka vitu vingi mno maishani mwake. Choyo aliyokuwa nayo ilimfanya adanganyane na kuiba.

Baada ya Zakayo kukutana na Yesu aliaibika kwa choyo aliyokuwa

lilipokuwa linakuchwa watu waliwaleta wagonjwa wao kwa Yesu. Aliwaponya wote.

Sasa ilikuwa ni wajibu wa watu kuchagua kama watapokea madai ya Yesu au kukataa mambo aliyosema. Watu wa Nazareti walichagua kumkataa Yesu.

Uliza: Watu wengi Kapernaumu walimfikirije Yesu? (Waruhusu wanafunzi wazungumze jambo hili.) Kwa sababu walimwamini Yesu, walimkaribisha mjini kwao. Yesu alifanya miujiza mingi kwa sababu watu wa Kapernaumu walikuwa na imani kwake. Hapa pana maswali mazuri ya kujuliza sisi wenyewe.

Je, ninayaamini madai yake Yesu?

Je, naamini kwamba Yesu ndiye Masihi aliyetumwa na Mungu kuwa Mwokozi wangu?

Je, naamini kwamba anao uwzo wa kuponya roho zenye huzuni?

Je, namkaribisha Yesu kwa sababu nayaamini madai yake?

KAZI YA KUFANYA

1. Taja mji ambamo Yesu alilewa. Nazareti

2. Tafuta jambo Yesu alilofanya katika mji huo. Kata kifungu kisicho cha kweli.

a. Yesu alisimama kusoma maandiko hekaluni.

~~b. Hikuwani desturi yake Yesu kwenda hekaluni kila siku.~~

c. Yesu alisoma kutoka kitabu cha nabii Isaya.

3. Yesu aliwambia watu kuwa ni yeye ndiye aliyeandikwa habari zake nabii huyo. Weka alama hii (X) kwenye mstari iliyokando ya kifungu kinachoeleza jinsi watu walivyopokea habari hizo.

a. X Waliuliza, "Huyu siye mwana wa Yusufu?" (Walikuwa na maana kwamba waliwajua wazazi wake na hakuwa tofauti na wao.)

b. Waliamini kwamba Yesu alikuwa akaisema kweli.

4. Mungu alimtuma Elisha kumponya mtu ambaye hakuwa Muyahudi.

Piga mstari chini ya jina la mtu huyo.

Yona Naamani Isaka

Yesu aliondoka Nazareti akaenda Kapernaumu. Huko alikutana na mtu aliye kuwa mwenye roho ya pepo mchafu. Weka alama hii (X) katika vifungu vya sentensi za kumalizia zilizo sawa.

Mtu yule aliye kuwa mwenye pepo mchafu alikuwa () mashuani (X) sinagogini () nyumbani

Yule pepo mchafu alisema kwamba Yesu alikuwa () nabii (X) Mtakatifu wa Mungu

Yesu alimkanya au alimkemka yule pepo mchafu, akasema, () "Ulisema uongo!" (X) "Fumba kinywa, umtoke." () "Omba."

Mji mzima watu walikuwa wakiongea habari za uwezo wa Yesu. Chini ya kila picha andika hadithi

inayosimuliwa kwa kuangalia picha hiyo.




Yesu atawahubiri maskini Injili.
Yesu atawapa vipofu kuona.
Yesu atawapa watu kuwa huru.

~~Yesu atajitihiana na watu matajiri.~~


KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Alikuja kwake, wala walio wake hawakumpokea. Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake." Yohana 1:11-12

Ni rahisi kwetu kuona kwamba vifungu hivi vinatambua tofauti iliyokuwa kati ya watu wa Nazareti na watu wa Kapernaumu katika kumpokea Kristo. Pia vinatueleza jinsi watu wa ulimwengu wote wanavyosikia na kuwa na mawazo tofauti kuhusu habari ya kuja kwake Kristo. Watu wengi husikia maneno ya Kristo na kukata shauri kwamba hawahitaji maneno hayo. Lakini watu wengi waamini na kumpokea Kristo kama Mwana pekee wa Mungu. Wakati waja kwa kila mmoja kulazimika kukata shauri hili. Je, wewe utakata shauri kwa njia gani?



Miaka mingi kabla ya Yesu kuanza kazi yake, nabii Isaya alisema kwamba Mashihi atakuja. Isaya alisema hasa kile Yesu atakacho fanya. Soma Luka 4:18-19. Halafu kikatika kifungu kisicho kwele.



HATI YA KUVIRUNGISHA

alikuwa mkubwa wa watoza ushuru. Twaweza kuona mfano jinsi Zakayo alivyokuwa kwa kutumia fikiria zetu. Hebu tuchanie kwamba taifa moja adui lilishinda lingine. Kisha adui hao wakamchagua mtu mmoja wa taifa ilie walioshinda kuwa mkubwa wa watoza ushuru kutoka kwa watu wake na kuvapelekea mtu huyu anayewatoza wenzawe ushuru na kuwapa adui atachukuliwa kama msaliti wa taifa lake. Watu wote watamchukia.

Na je, kama mtu huyu akikusanya fedha zaidi ya kiasi kile kinachohitajiwa na adui, na kujitajirisha kabisa kwa fedha hizo alizokusanya zaidi kwa hila, kutakuwa na nini?

Huu ndio mfano hasa wa Zakayo. Alitumikia taifa la kigeni, taifa la Warumi, na alikusanya ushuru kutoka kwa watu wa kabila lake, Wayahudi. Watu hawa wa kabila lake, Wayahudi, bila shaka alimchukia! Hakuna ye yote aliyeweza kumsalinia alipopitia njiani.

Zakayo alikaa Yeriko, mji ambao ni kilometa 25 upande wa mashariki ya Yerusalemu. Mji huu ndio uliokuwa makao makuu ya watoza ushuru wa mapato na hata wa forodhani. Zakayo alikuwana kazi muhimu sana. Alikuwa mkubwa wa watoza ushuru.

Hadithi yetu juu ya Zakayo inapalikana katika Luka 19:1-10.

(Mwambie mwanafunzi mmoja asome vifungu hivyo vya maandiko.)

Ifuatayo ni hadithi hiyo.

Siku moja Zakayo alisikia ya kwamba Yesu alikuwa akishuka miji kwa. Labda alikuwa amekwisha kuuja ya kwamba Yesu alikuwa mwenye huruma kwa watoza ushuru na wenge dhambi wengine ambao hawakufutata sheria za Mungu. Basi, Zakayo akakata shauri kwamba atakwenda kumwona mtu huyu ambaye watu wengi walimwita "Mwalimu." Labda Zakayo alitaka kitu ambacho fedha zake zote hazikuweza kununua.

Je, ni gani kilichomzuia Zakayo kumwona Yesu? Ndiyo. Alikuwa mfulupi wa kimo na hakuweza kumwona Yesu kwa sababu ya umati wa watu waliomfuata Yesu. Lakini Zakayo hakufa moyo. Alitangulia mbio mbele ya umati akapanda mti. Alikaa hapo mlini akamngojia Yesu kupitia pale.



Mwishowe aliweza kumwona Yesu akija kwa njia ile huku akiwa amezungukwa na umati wa watu. Yesu alipofika karibu na mti ulc alisimama, akamtazama Zakayo juu ya mti ulc. Labda Zakayo alishangaa mno Yesu alipomwita kwa jina lake hasa na kumwambia kwamba atakwenda naye nyumbani kwake na kula naye.

YESU AMWOKOA MTU ALIYEKUWA MTINI

MASOMO YA BIBLIA: Luka 19:1-10

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Tukiwa watu wa Bwana Yesu, Baba Mungu wetu anataka tuwe kama Yeye. Mungu atwambia vile anavyotaka tuishi katika Neno lake. Labda inaweza kudhaniwa kuwa ni rahisi kufuata maongozi ya Mungu, lakini si rahisi. Kila siku tunajaribiwa kutenda dhambi katika mambo madogo na kutomfuata Mungu kamili.

Labda twaweza kutambua dhambi nyingi na kuepukana nazo, lakini wakati mwingine Shetani hutumia njia za hila kutujaribu. Tujihadhari na jambo hili maishani mwetu na kutumia nafasi hii leo kuwaonyesha watoto jinsi tunavyoweza kujaribiwa kufanya dhambi.

Kristo ana uwezo wa kugeuza maisha yetu kabisa. Wakati tunapompokea katika maisha yetu, yeye hutaka kutusaidia kuishi maisha yasiyo na dhambi. Somo la siku hii latusimulia hadithi ya mtu mmoja ambaye maisha yake yaligeuzwa kabisa kwa uwezo wa Yesu.

Walakini, Mungu akiwa anaweza kumgeuza mtu huyu mwenye dhambi na kumfanya kuwa mtu mpya, kwa kweli aweza kutufanya hivyo hata sisi pia. Mtu huyu, Zakayo, alikuwa mtu ambaye alikuwa na dhambi moja kuu. Hakuwa mwaminifu. Walakini, Yesu

alipomgeuza alipata tamaa ya kutaka kuishi kwa uaminifu.

Unapofundisha, kumbuka kusudi hizi mbili: (1) kuwaonyesha wanafunzi wetu kwa somo hili kwamba wote ambao wanamweka Kristo kwanza maishani mwao wanataka kuishi maisha ya uaminifu, na (2) kuwaongoza wanafunzi wetu kuwa na tamaa ya kumweka Kristo kwanza maishani mwao kwa kuishi maisha ya uaminifu.

MAMBO YA KUKAZA

1. Yesu, ambaye alikuwa tofauti na viongozi wa kidini wa wakati ule wake, aliwapenda hasa wale ambao waliitwa wenye dhambi.

2. Yesu ana uwezo wa kugeuza kamili maisha ya wale wanaomwamini hasa. Ugeuzi huu unaleta furaha.

3. Yatupasa kuonyesha kwa uaminifu wetu kwamba maisha yetu yamekwisha geuzwa, ikiwa tumekwisha kumwamini Kristo kweli na kumweka kwanza katika maisha yetu.

KULIFUNDISHA SOMO

Leo tutajifunza habari za mtu mmoja aitwaye Zakayo. Jina lake maana yake ni "msafi" au "mwenye haki." Je, alishi kama vile jina lake linavyosema? La. Alikuwa mtoza ushuru asiye mwaminifu na ambaye alichukiwa sana. Na zaidi ya hayo,

WAKATI WA KUFUNGA

Labda utapenda kufunga somo hili kwa kuwaongoza wanafunzi wako kuimba pamoja. Pengine wajua wimbo ambao utakusaidia kutilia mkazo mambo muhimu ya somo hili, au yale muhimu ya masomo haya ya miezi mitatu. Jambo letu muhimu katika somo hili, ni "kumweka Kristo kwanza maishani mwetu."

Wanafunzi wako wamekwisha pewa nafasi ndani ya vitabu vyao kuandika jibu lao kama watampokea au kumkataa Kristo. Waweza kuwasaidia kuona kuwa hili ndilo swali muhimu kujibu kuliko swali lingine.

Waweza kuwasaidia ili wamchague Kristo maishani mwao. Ukitaka, waweza kutenga nafasi fulani kwa wanafunzi wako kudhihirisha chaguo lao mbele yako na mbele za wenzao wa darasani. Usijaribu kuwalazimisha kukata shauri.

Ikiwa utafunga somo kwa maombi, labda utapenda kuomba ili kwamba wewe na wanafunzi wako mwe tayari kwa jambo lo, lote atulizalo Kristo, na kwamba tutampa nafasi ya kwanza maishani mwetu. Waombee wale ambao wamekwisha kukata shauri kumkataa Kristo kama Mwana wa Mungu.

YESU AFANYA MIJIZA ZIWANI

MASOMO YA BIBLIA: Luka 5:1-11

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Katika somo hili utawaongoza wanafunzi wako kuuliza, "Nawezaje kumpa Kristo nafasi ya kwanza maishani mwangu?" Hakuna hadithi kuu ya kueleza swali hili kuliko hadithi ya Petro alivyomjua Yesu na kuacha kila kitu na kumfuata.

Kukutana kwa Petro na Yesu kulifanya mabadiliko makubwa maishani mwa Petro. Fikiri kwamba ilikuwa ajabu gani kukutana na mtu mwenye uwezo mkuu kama Yesu! Si vigumu kuamini kwamba Petro kwanza hakujua huyu mtu (Yesu) alikuwa nani. Walakini, Yesu alipomwanuru, Petro alijua kuwa yampasa kumfuata. Na akamfuata kweii.

Aliacha kila kitu ili kumweka Yesu kwanza maishani mwake. Aliacha biashara yake ya uvuvi akamfuata Kristo aliyemwahidi kwamba atamfanya kuwa mvuvi wa watu. Petro alikubali kutimiza mambo yote na hata zaidi, ili aweze kuwa pamoja na Kristo.

Thamani ya kumfuata Yesu ingali sawa hata siku hizi. Tukiataka kumfuata Kristo kama wafuasi wake, ni lazima tukubali kuacha kila kitu. Je, mwalimu, una nia ya kumpa Kristo nafasi ya kwanza maishani mwako? Ukiwa huna, basi hutaweza kuwaongoza wanafunzi wako kupata

furaha hii kuu. Kusudi la somo letu ni kuwaonyesha wawilana na wasichana kwamba wanaweza kumpa Kristo nafasi ya kwanza maishani mwao kwa kumtegemea awasaidie kuishi maisha ambayo Kristo ataka waishi.

Pengine hadithi ifuatayo itatusaidia kama mfano kutiwaonyesha vile tunavyoweza vitu vingine kuwa vya kwanza maishani mwetu.

Pele ni mzaliwa wa Brazil, taifa lililo katika Amerika ya Kusini. Alichaguliwa kama mchezaji mashuhuri wa mpira (kandanda) ulimwenguni. Alipokuwa kijana mdogo, alikata shauri kwamba siku moja atakuwa mtu anayejulikana na tena maarufu. Akaanza kufanya bidii ya kutimiza madhumuni yake. Alicheza mpira na kufanya mazoezi kwa saa nyingi hata akakosa kuwa na wakati wa kushirikiana na wenzake katika michezo. Alikata shauri kuacha mambo mengi aliyoyapenda mno kwa sababu ya ndoto yake ya kuwa mtu mashuhuri wa kandanda.

Baada ya miaka mingi ya mazoezi makali, Pele alianza kucheza mpira kwa timu yake ya Brazil. Muda si muda, akawa mchezaji mashuhuri kuliko wote katika Amerika Kusini. Katika mwaka wa 1968, Pele pamoja na timu yake, walisafiri hadi Mexico kushiriki katika mchezo wa mataifa yote ya ulimwengu. Alicheza kwa ustadi mno hata timu yake ikawa ndio

Weka alama hii (X) kwenye mstari ulio kando ya sentensi inayoonyesha zawadi ambayo Yesu aliwahidi wale ambao wanaacha nyumba zao na jamaa zao ili kumtumikia.

— Mali nyingi na heshima hapa ulimwenguni.

X Baraka nyingi hapa ulimwenguni.

X Uzima wa milele mbinguni.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Basi, kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu." Luka 14:33

Labda hatuna mali nyingi kama yule mtawala tajiri ambaye alikuja kwa Yesu, na labda Kristo hatawambia tuze mali chache ambayo tunayo. Walakini, ni lazima tuwe tayari kuacha vitu vyetu vyote vya kidunia tunapokuwa wanafunzi wa Yesu. Vitu hivi haviweza kuwa vya muhimu tena maishani mwetu.

Kumweka Kristo kwanza maishani mwetu kiwe kitu cha muhimu sana maishani mwetu wala siyo fedha au chakula au vifaa au jamaa. Je, uko tayari kumfuata Kristo ikiwa ni lazima uache vitu hivi vyote?

KULIFUNGA SOMO

Ujumbe wa somo hili ni wenye uwezo mkuu. Hadithi ya mtawala yule tajiri ambaye alikataa kuacha mali yake na kumfuata Yesu ndio mfano kwetu. Mara nyingi tunafanana na mtu huyu, na labda Yesu atwambia, "Mapungukiwa na neno moja bado."

Kwa kuwa tumejifunza masomo haya jinsi ya kumweka Kristo kwanza maishani, tumeona jinsi watu wengine waliyomweka Yesu kwanza katika maisha yao. Na sasa, tumekwisha kuona mambo aliyotwambia Yesu mwenyewe juu ya kumweka kwanza maishani mwetu.

Tuombe ili tuwe na nia ya kumweka Kristo kwanza juu ya vitu vyote katika ulimwengu huu wetu. Tumfanye kuwa Bwana wa maisha yetu.

Je, ni zavadi gani mtu anazopata kwa kumweka Mungu kwanza maishani mwake? Yesu alisema ya kwamba mtu ye yote anayemfuata hasa ana furaha halisi, amani na uradhi moyoni mwake katika maisha yake ya sasa, na katika ulimwengu ujao atapata uzima wa milele.

Kwa wiki nyingi tumekuwa tukizungumza juu ya kumweka Kristo kwanza maishani.

Je, kumweka Kristo kwanza maishani kulikuwa na maana gani kwa Petro, mwanafunzi wa Yesu? (Kwake kulikuwa na maana ya kuacha shughuli za kuvua samaki na kumfuata Yesu kila siku, na kutenda mambo ambayo Yesu alitaka.)

Je, kumweka Yesu kwanza maishani kulikuwa na maana gani kwa mtawala yule tajiri? (Kwake kulikuwa na maana ya kuacha utajiri wake wa kidunia na kumfuata Yesu kama mwanafunzi wake mnyenyekevu.)

Je, kumweka Kristo kwanza maishani mwako kuna maana gani kwako? Wataka kumweka kwanza mwaishani mwako? Kwa nini? Waweza kumweka kwanza maishani mwako?

KAZI YA KUFANYA

Katika picha iliyo hapo chini mtawala tajiri anamwuliza Yesu swali. Andika swali hilo ambalo mtu huyu alimwuliza Yesu.

Yesu alimwambia mtawala yule tajiri afanye mambo fulani kisha atakuwa na hazina mbinguni. Andika namba ya mambo hayo ambayo Yesu alimwambia kulingana na wakati alipoyasema.

3. Njoo unifuata.

1. Viuze ulivyo navyo vyote.

2. Ukawagawanyie maskini.

Chora duara kwa majina yaliyo hapo chini ya watu ambao Yesu alisema kwamba wana shida ya kuingia ufalme wa Mungu.


Wazee Maskini Wema
Wenye Mali Vijana Wenye Huzuni

Piga mstari chini ya jibu lililo sawa.

Yesu alisema kwamba ni vugumu kwa tajiri kuingia ufalme wa Mungu kuliko:

Chombo (merikebu) kuabiri katika nchi kavu.

Ngamia kupitia katika tundu la sindano.



Mwalimu nifanye nini
ili nipate kuirithi
uzima wa milele?

mabingwa wa kandanda ulimwenguni, naye akachaguliwa kama mchezaji mashuhuri katika ulimwengu. Ile ndoto yake ya zamani imetimika!

Je, kungefanyika nini kwetu kama tungemweka Kristo kuwa wa kwanza katika maisha yetu, kama vile Pele alivyoweka mchezo wa kandanda kuwa kitu cha kwanza maishani mwake? Hili ndilo jambo ambalo Yesu anatuuliza tufanye, na inatupasa kufanya bidii kumfuata Yesu kama vile Pele alivyofanya kuwa mwana kandanda mashuhuri katika ulimwengu.

MAMBO YA KUKAZA

1. Yesu alipoonyesha uwezo wake katika mwujiza ule wa kuwakamata samaki wengi, Petro alithibitishiwa hatia ya dhambi zake.

2. Yesu aliahidi kufanya mwujiza mwingine mkuu katika Petro, ili kumfanya kuwamvuvi wa watu.

3. Petro alimwitikia Yesu kwa kuacha mambo yote na kumfuata.

4. Thamani ya kuwa mfuasi wa Yesu siku hizi ni kama zamani. Yesu ni lazima awa wa kwanza maishani mwako.


KULTAYARISHA SOMO

Sema: Watu wengi walitaka kumwona Yesu. Walitaka kusikiliza neno la Mungu. Wakamitea wagonjwa awaponye.

Siku moja Yesu alitembea kando kando ya ziwa. Makutano ya watu wakamsonga! Pengine, Yesu alikuwa amechoka. Alikuja ulimwenguni

kuonyesha upendo wa Baba yake kwa watu WOTE. Hata alipochoka namna gani alitenda yale Baba yake alimtaka afanye.

Karibu naye kulikuwa na mashua mbili za kuvulia samaki. Wavuvi wanne walikuwa wanaosha nyavu zao baharini. Yesu alingia mashua ya Petro. Akamwambia, "Petro, tafadhali kipeleke chombo hiki mbali kidogo na pwani."



Watu wote sasa waliweza kumsikiliza kumwona Yesu vizuri. Baada ya Yesu kumaliza kuscma, alimcukia Petro, akamwambia, "Tweka mpaka kilindini, mkashushie nyavu zenu mvue samaki."

Petro alifikiri kuwa neno hili la Yesu ni la upuzi tu! Hakuna mvuvi yote yote mwenye akili anayeweza kuthubutu kushika samaki wakati wa mchana wa jua kali. Petro na mwenzake walivua usiku kucha wasiwaze kupata kitu. Na sasa Yesu alikuwa akimwambia ati akavue tena, na hali wakati wa mchana.

Sema: Bila shaka, mawazo ya Petro yalishindana, kwa sababu hakuna mvuvi ye yote mwenye akili ambaye angefanya jambo la upuzi kama hilo.

Lakini moyoni mwake hasa, Petro alijua ya kwamba Yesu alikuwa na uwezo wa kumwambia jambo la kufanya. Alijua kwamba aweza kumwamini Yesu. Na tena alikuwa na imani ya kwamba akiit, Yesu angeyarekebisha mambo yote.

Basi Petro akanjibu Yesu, "Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tuspate kitu. Lakini kwa neno lako nitazishusha nyavu."

Ni furaha gani waliyokuwa nayo wakati walipo shika samaki wengi na nyavu zao zikaanza kukatika? Petro aliwaita Yakobo na Yohana, akisema, "Njoni mtusaidie!" Mara moja wakaja, wakazishika zile nyavu zilizokuwa zikikatika kwa wingi wa samaki, wakajaza chombo chao pia.



Pengine hii ilikuwa ni mara ya kwanza maishani mwa Petro kushangaa. Mvujiza huu wa Yesu ulikuwa ni wa ajabu kwake. Basi awezaje mtu mwenye dhambi kama yeye kuwa rafiki wa Yesu ambaye alikuwa na uwezo wa ajabu kutoka kwake Mungu!

Petro alianguka magoini pa Yesu, akisema, "Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mwenye dhambi, Bwana!"

Uliiza: Je, Yesu aliondoka?

Lai! Haondoki kwetu wakati tunapozungama dhambi zetu. Ni wakati huo ambapo anjongea karibu nasi na kuondoa dhambi ambayo imetunga naye. Anapokwisha kutusamehe dhambi zetu, na tuwa wasafi, basi tuko tayari kufanya kazi yake.

Katika mpango wake mkuu, Mungu hakumtaka Petro kushusha nyavu zake na kuvua samaki. Huu ulikuwa mfano tu wa uvuvi wa ajabu ambao Petro angefanya baadaye - uvuvi wa watu.

Hakuna mtu aliyeona mvujiza ule ukianzia rohani mwa Petro, lakini bila kuwa na shaka, tuna hakika kwamba ulianzia hapo. Tunajuaje hivyo? Tunajua kwa sababu Petro aliacha vitu vyote, akamfuata Yesu.

Uliiza: Je, wafikiri kwamba Petro aliacha nini kumfuata Yesu na kuwa mfuasi wake? (Jaribu kuwafanya wanafunzi wako wazungumze juu ya vitu vile hasa ambavyo Petro aliacha alipomfuata Yesu. Alipata nini kwa kumfuata Yesu? Zungumza juu ya jambo hili.)

wanafahamu ya kwamba Mungu hataki kila mtu kutoa kama zawadi vyote alivyo nayo ili ndipo aweze kumfuata Yesu.

Yesu alikuwa amejijibu swali la mtawala, lakini hakufurahia jibu hilo. Alikuwa na swali lingine. Je, swali hilo hasa lilikuwa lipi ambalo yule mtawala alipaswa kujibu? Ndiyo, alipaswa kukata shauri kama atafanya kama alivyoambiwa na Yesu au kuendelea kuishi kama aliyokuwa akiishi zamani. Yesu hakusema ya kwamba ni dhambi kuwa na mali nyingi. Lakini alikuwa akisema kwamba ni dhambi kuthamani kitu kingine zaidi kuliko vile unavyomhamani yeye. Ni lazima umpokee kuwa wa kwanza maishani mwako.

Ni uamuzi gani ambao yule mtawala alufanya? Hakuweza kujipendeza yeye mwenyewe na kumpendeza Kristo pia. Alichagua kujipendeza mwenyewe. Alimwacha Yesu pale na akarudia utajiri wake kwa sababu hakuwa tayari kumweka Kristo kwanza maishani mwake.

Je, kisha Yesu alisema nini juu ya utajiri? Alisema kwamba ni rahisi kwangamia kupita katika tundu la sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu. Alikuwa na maana gani kwa maneno haya? Alikuwa na maana kwamba imani ilelayo wokovu na uzima wa milele ni imani ile imwekayo Kristo kwanza maishani, kabla likya mali. sindano ambavyo Yesu alizungumza ilikuwa tundu dogo katika kuta za mji ambalo watu walipitia wakati miango ilipofungwa

wakati wa jioni. Ngamia aliweza kupita katika tundu hili, lakini kwa juhudi kubwa. Mzigo wote alionbeba mgongoni mwake uliondolewa kabla ya ngamia kupita katika tundu hili ndogo.

Je, ni kwa nini wafikiri mali inawazua watu kujua kwa Kristo? Zungumza swali hili na wanafunzi wako. Wengi wetu si tajiri, lakini kuna vitu mbali na fedha, ambavyo tunaviweka kwanza maishani mwetu. Bwana ana masharti makubwa. Anatwambia tuache cho chote kinachotuzua kumfuata kwa moyo wetu wote. Lengo letu lafaa kuwa kumtii hasa.

Je, mtawala yule alipaswa kufanya nini ikiwa alitaka wokovu? Ilimpassa kumwamini Kristo kwanza. Angaliweza kuthibitisha imani yake ikiwa angalikubali kugawanya hazina yake na wengine.

Baada ya kusikia vile ilivyokuwa vigumu kwa watu wapendao mali kuingia mbinguni, wanafunzi walishangaa. Walikuwa wafikiri kwamba utajiri ndio uliokuwa thibitisho la upendo wa Mungu. Kwa hivyo walishangaa, wakasema, "Nii nani basi awezaye kuokoka?" Yesu aliwaonyesha ya kwamba ingawa mtu awezi kuokolewa binafsi kwa kazi yake nzuri, yasiyowezekana kwa mwanadamu yawezekana kwa Mungu. Yesu aweza kugeuza roho za wale awasafisha dhambi ili kwamba wampende Mungu kuliko fedha au kitu kingine cho chote. Upendo wake moyoni mwao utawafanya wawepende jirani zao pia.



Twajua mambo fulani juu ya mtu huyu. Mwanzo wa kifungu hiki unamtaja mtu mkubwa, na mtawala. Alikuwa na mamlaka ya kutawala. Kifungu cha 23 kinasema kwamba alikuwa tajiri. Hata siku moja, mtawala huyu alisikia kwamba Yesu alikuwa katika mji fulani. Alikwenda mbio kukutana naye. Na kwa kuonyesha heshima yake kwa mwalimu (Yesu), alipiga magoti mbele yake. Kisha akamwuliza Yesu swali ambalo lilikuwa likimsumbua sana rohani mwake.

Je, wafikiri kwamba waliokuwa wakisimama pale karibu nao walistaajabu kwa kusikia swali hilo lake? Watu wengi tajiri hawajali juu ya uzima wa milele. Lakini mali, elimu, utawala na hali ya mtawala huyu zilikuwa hazijamtocheleza. Alikuwa mwaminifu wa kutosha kwa kumwambia Yesu ukweli kwamba hakutosheka na vitu hivyo maishani mwake.

Yesu alijiibuje swali lake? Alimwambia, "Mbona unaniita mwema?"

Yesu alikuwa akimwuliza ni kwa nini alimpa cheo ambacho ni cha Mungu pekee. Ikiwa mtawala huyu alijua kwamba Mungu pekee ndiye mwema, basi pengine alikuwa akijaribu kumpendeza kwa kutii sheria zake. Kwa hivyo, Yesu alimkumbusha amri tano za Mungu.

Je, mtawala huyu alisema nini juu ya amri hizi? (Ndiyo, alisema kwamba alikwisha kuzitii amri hizo tangu utoto wake.) Alipozungumza na Yesu labda alifikiri kwamba ana nia ya kumtii Mungu kwa kila njia. Alifikiri kwamba ana nia ya kufanya vitu vyote ambavyo Mungu alimtaka atende. Lakini je, alikuwa na nia kweli?

Kwa kujaribu wema wa mtawala huyu, Yesu alimwambia afanye kitu fulani. Alimwambia auze vyote alivyo navyo na kuwagawanyia maskini fedha. Kama akifanya hivi, basi atakuwa na hazina mbinguni. Mtawala huyu pia aliambiwa na Yesu kwamba baada ya kuuza mali yake, aje amfuate.

Yesu hakuwa anasema hapa ya kwamba kila mtu ni lazima auze mali yake ili ndipo amfuate. Hii SI sheria ambayo kwayo watu wanaokolewa. Lakini, Yesu alikuwa akimjaribu mtawala huyu kwa sababu alikuwa na majivuno makuu katika mambo aliyotenda. Alifikiri kwamba aweza kupata wokovu kwa kazi zake njema tu. Utajiri wake ulimtenga mbali na Mungu. Hakikisha kwamba watoto

Vitu Petro alivyoviacha alipofuata Yesu:

mashua, biashara, nyumba, rafiki, kuwa bwana wa kibinafsi

Vitu Petro alivyopata kwa kumfuata Yesu:

kumjua Yesu, kuona uwezo wa Mungu, kubadilishwa kiroho na Yesu, furaha katika kumtii Yesu

Labda wewe hujui KWA NINI vapaswa kumpa Kristo nafasi ya kwanza maishani mwako.

1. Anipenda mno. Yesu akupenda mno hata akafa kwa ajili yako. Je, hutaki kujitoa? (Mwambie mwanafunzi mmoja asome Yohana 15:13.)

2. Mimi ni mali ya Kristo, alinunua kwa dhamani ya damu yake. Ukiwa umekwisha kumpokea Yesu kuwa Mwokozi wako, sasa u mali ya Mungu. (Mwulize mwanafunzi mmoja asome 1 Wakorintho 6:20.) Baada ya kwenda dukani na kununua kitabu kwa fedha zako mwenyewe, waweza kusema, "Kitabu hiki ni changu." Ikiwa kuna mtu anayebishana nawe, waweza kumweleza kwamba, "Nilikinunua mimi. Nilitoa fedha zangu nikakiliipia." Katika njia hiyo, Kristo aweza kukuambia wewe ukiwa Mkristo kwamba, "Wewe u mali yangu. Nilikununua. Nilikulipia deni lako la dhambi kwa damu yangu mwenyewe.

3. Ninakuwa na furaha kuu wakati ninapampa Kristo nafasi ya kwanza maishani mwangu. Yesu alisema

kuwa unapomtii, na unapomruhusu kuyatawala maisha yako, washiriki furaha yake. (Mwambie mwanafunzi mmoja asome Yohana 15:10-11.)

4. Ninapokiri kwamba Yesu, ambaye ni Mwana wa Mungu, ndiye Bwana, huwa ninamtukuza Mungu ambaye ndiye Muumba wangu. Vile tunavyoambiwa katika kifungu cha kukumbuka cha somo hili, yatupasa kumtambua Kristo kuwa ndiye Bwana wetu.

KAZI YA KUFANYA

Wiki iliyopita ulisoma juu ya miji miwili ambayo Yesu alitembelea. Kati ya hiyo miji miwili ni mmoja tu ambamo watu walifurahi kumsikiliza Yesu. Andika jina la mji huo hapa. Kapernaumu Kisha Yesu alikwenda kwenye ziwa kubwa. Biblia inatoa majina matatu ya ziwa hilo. (Yohana 6:1; Luka 5:1). Yaandike majina haya kwenye nafasi iliyoko hapa.

Bahari ya Galilaya

Bahari ya Tiberia

Genezareti

Watu wengi walitaka kujua zaidi juu ya Yesu. Siku moja, Yesu alipokuwa kwenye ziwa, makundi ya watu walimfuata. Andika jibu nzuri katika kila mstari.

Watu gani walimzunguka Yesu?

Walitaka kusikia nini?

Wavui walikuwa wakifanya nini?

Labda wewe hujui KWA NINI wapaswa kumpa Kristo nafasi ya kwanza maishani mwako.

1. Anipenda mno. Yesu akupenda mno hata akafa kwa ajili yako. Je, hutaki kujitoka? (Mwambie mwanafunzi mmoja asome Yohana 15:13.)

2. Mimi ni mali ya Kristo, alinunua kwa dhamani ya damu yake. Ukiwa umekwisha kumpokea Yesu kuwa Mwokozi wako, sasa u mali ya Mungu. (Mwulize mwanafunzi mmoja asome 1 Wakorintho 6:20.) Baada ya kwenenda dukani na kununua kitabu kwa fedha zako mwenyewe, waweza kusema, "Kitabu hiki ni changu." Ikiwa kuna mtu anayebishana nawe, waweza kumweleza kwamba, "Nilikununua mimi. Nitoea fedha zangu nikakilipta." Katika njia hii, Kristo aweza kukuambia wewe ukiwa Mkristo kwamba, "Wewe u mali yangu. Nilikununua. Nilikulipta deni lako la dhambi kwa damu yangu mwenyewe.

3. Ninakuwa na furaha kuu wakati ninapompa Kristo nafasi ya kwanza maishani mwangu. Yesu alisema kuwa unapomti, na unapomruhusu kuyatawala maisha yako, washiriki furaha yake. (Mwambie mwanafunzi mmoja asome Yohana 15:10-11.)

4. Ninapokiri kwamba Yesu, ambaye ni Mwana wa Mungu, ndiye Bwana, huwa ninamtukiza Mungu ambaye ndiye Muumba wangu. Vile tunaayoambiwa katika kifungu cha kukumbuka cha somo hili, yatupasa

kumtambua Kristo kuwa ndiye Bwana wetu.

KAZI YA KUFANYA

Wiki iliyopita ulisoma juu ya miji miwili ambayo Yesu alitembelea. Kati ya hivyo miji miwili ni mmoja tu ambamo watu walifurahi kumsikiliza Yesu. Andika jina la mji huo hapa. Kapernaumu Kisha Yesu alikwenda kwenye ziwa kubwa. Biblia inatoa majina matatu ya ziwa hilo. (Yohana 6:1; Luka 5:1). Yaandike majina haya kwenye nafasi iliyoko hapa.

Bahari ya Galilaya

Bahari ya Tiberia

Genezareti

Watu wengi walitaka kujua zaidi juu ya Yesu. Siku moja, Yesu alipokuwa kwenye ziwa, makundi ya watu walimfuata. Andika jibu nzuri katika kila mstari.

Watu gani walimzunguka Yesu?

Walitaka kusikia nini?

Wavuvi walikuwa wakifanya nini?

Yesu alifundisha akiwa wapi?

majibu: katika chombo cha kuvulia samaki, watu wengi, Neno la Mungu, wakiosha nyavu.

Jibu maswali yafuatayo.

Kama ungekuwa Petro ungemitii Yesu?

Kwa nini?

Sura ya Kumi na Moja

YESU AELEZA JINSI YA KUMWEKA KWANZA MAISHANI

MASOMO YA BIBLIA: Luka 18:18-30

KUJIANDAA KUFUNDISHA

"Umepungukiwa na neno moja bado." Maneno haya Yenye kubabaisa yaliambiwa tajiri. Alikuwa mtu mwema. Labda watu wote katika kijiji chao walitamani kuwa kama yeye. Alikuwa na vitu vyote ambavyo mtu aweza kuhitaji katika kujiburudisha maisha yake. Alikuwa na mali, na aliweza kununua kitu cho chote alichotamani. Lakini hata hivyo, alipungukiwa na kitu kimoja. Hakuwa na nia ya kumweka Kristo kwanza maishani mwake. Bila kitu hiki kimoja, vitu vyote aliyokuwa navyo havikuweza kumfanya kuwa na furaha.

Mara kwa mara twafikiri kwamba tuna vitu vyote tunayohitaji kwa kuwa na nyumba nzuri, nguo nzuri, chakula na pengine fedha. ara nyingi twafikiri ya kwamba kuwa na vitu hivyo ndiyo "maisha." Yesu alitonyesha kwa hadithi hii ya leo kwamba tunakosa kufikiria hivyo. Kristo alisema ya kwamba alikuwa amekujia ili kwamba tuweze kupata uzima wa milele, ili kwamba tuweze kuupata uzima huo kwa wingi zaidi. Hakusema kwamba alikuja na kufa msalabani ili tuweze kupata yakula vingi, au nyumba nzuri, au baiskeli. Alikuwa na maana kwamba alikuwa amekujia kutupa vitu vya maisha ambavyo ni vya muhimu sana.

Mara kwa mara vijana hawajui vitu vya maisha ambavyo ni vya thamani kubwa kuliko nyingine zote. Mara nyingi wanachanganyikiwa katika kutafuta majibu. Wewe kama mwalimu, una wajibu wa kuwasaidia wanafunzi wako kuona kwamba vitu vya muhimu hasa maishani ni vile ambavyo si vya kidunia, bali vya kiroho. Kusudi la somo hili ni kuwatia wanafunzi moyo kumweka Kristo kwanza maishani mwao.

Je, umekuwa ukionba ili kwamba Roho Mtakatifu awafundishe wanafunzi wako kwa masomo haya kutoka kitabu hiki? mba kwa jibu ili kwamba Bwana awe akkuongoza wakati unapojaribu kuwaongoza wanafunzi wako kumpa Kristo nafasi ya kwanza maishani mwao.

MAMBO YA KUKAZA

1. Mali, kazi nzuri, na kuishi kwema hakutoshelezi roho zetu.

2. Masharti ya Yesu kwa mtu kuwa mwanafunzi wake yalionekana magumu kwa kijana yule tajiri.

3. Dhambi ni kuruhusu kitu cho chote kutuzuia kumweka Kristo kwanza maishani mwetu.

KULIFUNDISHA SOMO

Siku moja, mtawala mmoja tajiri alimwuliza Yesu swali muhimu sana. Aliuliza, "Mwalimu, nifanye nini ili nipate kuurithi uzima wa milele?" Swali hili linapatikana katika Luka 18:18.

na wakati ambapo twataka kuzungumza na Bwana.

Na sasa, kwa kuwa umefika wakati wa kufunga somo hili, labda utachagua kulifunga kwa maombi yako mwenyewe. Je, utamwomba Mungu jambo gani?

Hebu fikir juu ya mashindano yaliyokuwa katika mawazo ya Petro! Imani yake na akili yake yalikuwa na vita vikali. Ni kipi kilishinda vita hivyo? (Imani) Yesu alikuwa akimfundisha Petro kwamba, "Mambo yasiyowezekana kwa mwanadamu yawezekana kwa Mungu."

Yakate maneno yasiyo sawa katika vifungo.

Samaki walingia wavuvi hata ukaanza (kukatika) (~~kutataka~~).

Kwa hivyo wale watu waliwaita (Yakobo na Yohana) (Yesu) kuja kuwasaidia.

Baadaye Yesu alifundisha kundi lingine la watu. Piga mstari chini ya kifungu kinachoeleza maana ya mafundisho ya Yesu.

"Mwaweza kuwa wanafunzi wangu mkiishi maisha bora zaidi."

"Hamwezi kuwa wanafunzi wangu msipojitoa na vyote mliyonyavyo kwangu."

Baada ya Yesu kuwahubiria watu neno la Mungu alimpa Simoni Petro amri ya ajabu. Andika "K" kwa kweli au "M" kwa makosa mbele ya vifungu hivi.

M Yesu alimwambia Simoni kusogeza mashua yao karibu na ukingo wa bahari

K Wanaume hao walikuwa wamevua samaki usiku kucha bila kupata kitu.

K Simoni Petro alimtii Yesu kwa kushusha wavu kilindini.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

Na kila ulimi ukiri ya kuwa Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba. Wafilipi 2:11

Mpango wa Mungu kwa wanafamu wote ni kwamba sisi sote tutamwamini Yesu Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu. Awataka watu wanaoamini Mungu wasio wa kweli kuacha kuwaamini, bali wamtafute Kristo. Mpango wa Mungu ni kwa kila mtu kupata wokovu. Na kwa saba Baba yetu ni Mungu wa upendo, hataki hata mmoja wetu kufa katika dhambi.

Lakini mwanadamu amepewa akili ya kujichagulia mwenyewe kile atakachofanya na maisha yake. Mungu hamshurutishi mtu ye yote kumchagua Kristo maishani mwake. Petro hakushurutishwa kamwe kumwamini Mungu. Bali yeeye mwenyewe alikuwa na imani kisha akaamini. Kisha akazunguka huku na huku akiwaambia watu habari zake Yesu. Alikuwa akishuhudia ya kwamba Yesu Kristo ndiye Bwana. Alifanya hivyo kwa utukufu wake Mungu.

WAKATI WA KUFUNGA

Uliza: Ni jambo lipi ambalo ni la kwanza maishani mwako?

Ni jambo lipi ambalo ni la muhimu sana kwako?

Yesu Kristo asema kwamba tukimwamini kuwa ndiye Bwana, twamfanya kuwa mtu wa muhimu zaidi kuliko mwingine maishani mwetu. Mara nyingi tunakosa

kufanya hivi. Kumbuka vile Pele alivyotumia nguvu na uwezo wote ili awe mwana-kandanda mashuhuri. Je, sisi pia tu tayari kutumia nguvu na uwezo wetu ili tuweze kumtumikia Kristo katika njia inayofaa? Mungu ataka tumweke au tumpe nafasi ya kwanza katika mambo yote. Twahitaji kumpa nafasi ya kwanza katika ibaeda yetu, upendo, uti na katika utumishi wetu kwa wengine.

Unapofunga kwa maombi, utahitaji kumwomba Mungu awasaidie, wewe pamoja na wanafunzi wako, mwe kana Petro ambaye aliacha maishani mwake. Wawaombe pia watu wengi wa ulimwengu ambao hawajamkiri Yesu kuwa ndiye Bwana.

6 Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mnovu.

2 Ufalme wako uje.

4 Utupe leo riziki yetu.

1 Baba yetu uliye mbinguni, jima lako litukuzwe.

Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele, Amin.

Baba walezi (baba wa hapa ulimwenguni) wa watoto hawapi watoto wao vitu ambavyo vitawadhuru. Chora mstari kutoka kwa kila swali hadi kwa jibu lililo sawa.



Ni nini ambacho baba hatampa mtoto wake anayemwomba mkate?



Ni nini ambacho baba hatampa mtoto wake anayemwomba samaki?



Ni nini ambacho baba hatampa mtoto wake anayemwomba yai?

Yesu aliwaambia wanafunzi wake hadithi juu ya msafiri mmoja. Andika jibu lililo sawa katika nafasi hiyo iliyo hapo chini.

Usiku moja wamane, mtu mmoja alibisha mlango ni mwa jirani yake. Alitaka kukopa mikate kwa sababu mgeni alikuja kwake naye hakuwa na chakula.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaone; bisheni, nanyi mtatunguliwa." Luka 11:9

Mara nyingi tunakosa kupokea vitu kwa sababu hatuombi. Hadithi ambazo tunekwisha soma na kujifunza katika somo hili, zinatukumbusha ya kwamba Mungu, Baba yetu aliye mbinguni atatupa vitu vingi zaidi vyema ikiwa tutamwomba.

Sikuzote yuko tayari kutupa maisha mema zaidi tukimwomba. Hivi siyo kusema kwamba tukionba Bwana, atatupa fedha nyingi au vyombo, au vitu vingine. Vitu hivi si vya muhimu zaidi kuliko vyote maishani mwetu. Mungu anazo baraka nyingi kwetu sisi. Mara nyingi baraka hizi ni za kiroho.

KULIFUNGA SOMO

Maombi ni nini? Je, ni maneno tu tunayotunga wakati tunapokuwa na hitaji la kumwomba Mungu kitu? La, maombi yana maana zaidi ya mambo hayo. Maombi ni mazungumzo kati yetu na Mungu wakati ubalimbali. Mara nyingi twafikiri tu kuzungumza na Mungu wakati tunapohitaji kitu.

Mungu ataka tumwende wakati wa furaha, wakati wa shukrani kwa jambo fulani, wakati wa shida ambazo hatuwezi kuzisuluhisha sisi wenyewe,

wanawe wanaomjia mara kwa mara haki zaidi! Mungu atutaka tumwende mara kwa mara. Katika Luka 18:9-14 Yesu aliwasimulia hadhithi watu waliojifikiria kuwa ni wema kuliko wengine.

Alisema watu wawili walipanda kwenda hekaluni kuomba. Mmoja alikuwa Farisayo. Na wa pili alikuwa mtoza ushuru. Yule Farisayo akasimama akiomba, "Ee Mungu, nakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine. Mimi si mnyang'anyi wala mdanganyifu, wala mimi si kama huyu mtoza ushuru. Mimi nafunga mara mbili kwa juma badala ya mara moja kama vile inavyotakiwa na sheria ya Agano la Kale. Natoa zaka katika mapato yangu yote kwa Mungu."

Lakini mtoza ushuru alisimama mbali, wala hakuthubutu hata kuinua macho yake wakati wa kuomba. Maombi yake yalikuwa hivi, "Ee Mungu, uniwic radhi mimi mwenye dhambi."

Je, ni maombi yapi ambayo yalimpendeza Mungu zaidi? Yesu alisema ya kwamba mtoza ushuru aliondoka hekaluni dhambi zake zikiwa zimesamehewa. Alikuwa ameomba kwa unyenyekevu akitaka msamaha, na Mungu akayajibu maombi yake. Yule Farisayo hakuomba msamaha, na hakuamehewa.

Yesu alifundisha ya kwamba Mungu atajibu maombi yetu tukitubu dhambi zetu, natukiwa wanyenyekevu. Yatupasa kumpendelea Mungu katika kila hali ya maisha yetu.

Kutokana na masomo haya, twaona ya kwamba Mungu atutaka tuombe kwa juhudi, tuombe bila kuchoka, na kuomba kwa unyenyekevu. Je, tuwe tukiomba kwa kutaka nini? Je, wamjua mtu fulani aliye na hitaji? Je, wamjua mtu ambaye amepotea kiroho? Je, kunaye mtu karibu nawe ambaye anahitaji jirani mwema? Je, kuna mtu fulani unayemfahamu ambaye ahitaji msaada katika jambo analolifanya?

Je, kujua kuomba peke yake kunatosha? La. Tudhanie kwamba mama yako amekwisha kukufundisha namna ya kupika chakula. Hata siku moja akawa ameondoka nyumbani. Nawe wasikia njaa zaidi na kuona chakula karibu nawe, lakini hakijapikwa. Nawe "wajua" kupika.

Je, kujua kwako kupika kutakufanya usisikie njaa? La, ni lazima upike hasa chakula na kukila iwapo wataka ushibe. Kujua jinsi ya kuomba ni kuzuri, na tena ni jambo la thamani, lakini kutakusaidia tu ikiwa utaomba wewe mwenyewe.

KAZI YA KUFANYA

Yesu alitupa mfano wa sala tunaaita "Sala ya Bwana." Soma sala hii (Mathayo 6:9-13) halafu andika namba moja hadi saba katika nafasi zilizoachwa kuonyesha vile sentensi hizi zinafaa kufuatana.

5 Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu.

3 Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.

YESU NI TABIBU WA AJABU

MASOMO YA BIBLIA: Luka 5:12-26; 17:11-19

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Tunapoendelea na kichwa kisemacho "Kristo kwanza," utaona ya kwamba baadhi ya wanafunzi wako kwa kweli wanajaribu kumweka Kristo katika maisha yao hasa. Pengine wao ni kama Mkristo mchanga aliyesema, "Sikujuu kuwa nilikuwa mchoyo mpaka nilipojaribu kumweka Kristo kuwa wa kwanza maishani mwangu."

Tukitaka kumweka Kristo kwanza maishani mwetu, basi itatupasa kujifunza mengi juu yake. Somo la siku hii linaonyesha uwezo alokuwa nao Kristo katika kuwaponya wagonjwa. Kichwa hiki cha somo hili kisemacho "Yesu ni Tabibu wa Ajabu" kinatambua uwezo wa ajabu alokuwa nao kuwaponya wagonjwa. Tutaangalia hadithi tatu kati ya hadithi za watu waliomjia Yesu kuwaponya. Tutaona jinsi Yesu alivyowaonea upendo na huruma.

Hata wakati wa kuponya, Yesu alionyesha kwamba alikuwa amekuja kutimiza unabii uliotolewa kwamba Masihi atakuja. Tena wiki hii, twaona ya kuwa Yesu alifuata mafundisho ya Agano la Kale na kujajua sawasawa. Alijua sheria za Maandiko hayo na kuzifuata. Katika somo la leo tutaambiwa jinsi Yesu alivyomponya yule mtu mwenye ukoma. Ali-mwambia akajionyeshe kwa kuhani,

na kuleta sadaka ya kutakasika kwake. Uthitaji kusoma Mambo ya Walawi 14:2-32 ili upate kujua zaidi juu ya mafundisho hayo ya Agano la Kale ambayo ni ya Musa.

Kusudi la somo hili ni kuwaonyesha wanafunzi wako ya kwamba wanaweza kumwona Kristo akifanya kazi maishani mwao wakimwamini.

MAMBO YA KUKAZA

1. Yesu alionyesha huruma na aliwaponya wale waliomjia ili awaponye.
2. Kwa sababu Yesu ni Mwana wa Mungu, anao uwezo wa kusamehe dhambi na kuponya roho.
3. Yesu, ambaye ni Tabibu wa Ajabu, atupa uzima wa kiroho tunapomwamini na kumtii.

KULIFUNDISHA SOMO

Uliza: Je, Yesu anao uwezo ule ule wa kutusaidia kama alivyokuwa nao nyakati zile za Biblia?

Twajuaje ya kwamba Yesu aweza kuponya magonjwa? (Waache wanafunzi watoe majibu, kisha uendeleee.)

Sema: Twaweza kujifunza kutokana na miujiza mitatu ya Yesu.

Katika mji mmoja wa Palestina kulikaa mtu mwenye huzuni na mateso maishani mwake. siku fulani mbeleni, alikuwa ameona upele juu

ya ngozi ya mwili wake. Mara akatambua dhahiri kwamba alikuwa na ugonjwa ambao hakuna daktari aliyeshi wakati huo wa Biblia ambaye angeweza kuutibu.

Ukoma ulikuwa ugonjwa mbaya sana ambao uliambukiza mwili wote wa mtu. Kuambukiza kwake mwili kunaacha vidonda mwilini, na kuyala nyama za vidole, miguu, puu au vungo vingine vya mwili. Watu waliugopa sana ugonjwa huo hata hawakupenda kukaa na mtu huyu mwenye ukoma. Watu wasio wagonjwa walipomkaribia mtu huyu, alilazimika kupaza sauti na kusema, "Najisi, najisi!"

Mtu huyu alikuwa mgonjwa kwa muda fulani kwa sababu kwasoma katika Maandiko ya Biblia kwamba alikuwa ameambukizwa mwili wote. Habari za mwujiza wa ajabu wa Yesu ulipomfikia mtu huyu mwenye huzuni, aliwaza moyoni mwake kwamba pengine Yesu aweza kumsaidia.

Siku moja, mtu huyu mwenye ukoma alisikia habari kwamba Yesu alikuwa katika mji mmoja wa karibu. Alimwendea kwa haraka. Na kwa heshima akaanguka kifudufudi mbele ya Yesu. Alitaka sana msadaa kutoka kwa Yesu. Akasema, "Bwana, ukitaka waweza kunitakasa." Hakuwa na shaka kwamba Bwana hana uwezo wa kumponya. Lakini kulikuwa kitu kimoja ambacho hakujua. Hakuwa na hakika kwamba Yesu alitaka kumponya. Yesu angeweza kumponya. Je, angefanya hivyo?

Yesu, kwa upendo mkuu, aliuonyosha mkono wake, akamgusa.

(Mwulize mmoja kati ya wanafunzi wako asome maneno aliyoyasema Yesu katika Luka 5:13.) "Nataka. Takasika." Mara ukoma wake ukamwondoka, akawa mzima tena.

Yesu alimwaamuru mtu huyo asimwambie mtu ye yote juu ya mwujiza huu. Alimwambia akaji-onyeshe kwa kuhani, akatoe sadaka na kupokelewa kuwa ametakasika kabla ya kujunga na wengine. Lakini mtu huyo alikuwa na furaha kuu mno hata akaenda na kuwaambia wengine, na habari hizi njema zikaenea mjini kote.

Miezi mingine baadaye, Yesu alikutana na watu wengine kumi wenye ukoma. Wakapaza sauti zao kwa mbali wakisema, "Ee Yesu, Bwana mkubwa uturehemu."

Uliza: Je, wafikiri kwamba watu hawa walitaka Yesu kuwafanyia nini? Walitaka Yesu awaponye.)

Yesu alipowaona aliwaambia, "Enendeni, mkajionyeshe kwa makuhani." Amri hii ya Yesu pengine ilionekana kuwa upuzi kwa watu hao. Kwa nini wajionyeshe kwa makuhani kabla hawajaponywa? Lakini wailitwenda bila kumwuliza Yesu maswali. Yesu alikuwa amewaambia waende. Bila shaka, maana ya agizo hilo lake ni kwamba angewaponya. Ni kwele! Walipokuwa njiani, mlii yao iliponywa ikawa misafi tena.

Yesu alikuwa amewapa wenye ukoma hao zawadi isiyu na thamani kwa kuponya mlii yao. Lakini, kati ya watu hao kumi wenye ukoma, ni mmoja tu ndiye aliyerudi kumshukuru

Baada ya Yesu kumaliza kusimulia hadithi hii, alisema maneno ambayo ni ya kifungu chetu cha kukumbuka, Luka 11:9. (Labda utapenda kufundisha kifungu hiki cha kukumbuka sasa kuliko kungojea kukifundisha baadaye.)

Waomba kwa kutaka nini? Ndiyo, kitu cha hitaji.

Watafuta kwa kutaka nini? Kitu ambacho umekipoteza.

Unabisha kwa kutaka nini? Kwa kutaka mlango uliofungiwa ufunguliwe.

Je, kuna kitu unachotaka ambacho wafikiria kuwa Mungu akutaka uwe nacho? Yesu alisema, "Ombeni nanyi mapewa." Je, umepata kufanya kosa na kupoteza furaha yako? Yesu alisema, "Tafuteni, nanyi mtaona." Ukitafta msamaha wake, hukuasamehe mara moja. Je, kunacho kitu ambacho ni kama mlango uliofungiwa, yaani, kitu ambacho Mungu akutaka ufanye lakini wewe huwezi? Yesu alisema, "Bisheni, nanyi mtafunguliwa."

Kisha Yesu akasema, "Ukimwomba baba yako mkate, je, atakupata jiwewe? Ukimwomba baba yako chakula, je, atakupata kitu ambacho hakiwezi kuliwa?" Kwa kwele, la. "Mwana akimwomba babaye samaki, je, atampa nyoka? Au akimwomba yai, atampa nge?"

Yesu alitupa maswali haya ili kuonyesha kwamba, ikiwa wao, ambao ni waovu, wanajua kuwapa wana wao vitu vyema, basi Baba yao aliye mbinguni atawapa wale watu

wanwombao vitu vizuri zaidi kuliko vile.

(Hadithi mbili zifuatazo hazimo ndani ya vitabu vya wanafunzi, lakini zitaokusaidia wewe kama mwalimu kuelewa zaidi maana ya maombi au sala. Ukiwa una nafasi, labda waweza kuzitumia wakati unapofundisha.)

Baadaye Yesu aliwasimulia wanafunzi wake hadithi nyingine ili kuwafundisha juu ya maombi. Hadithi hii inapatikana katika Luka 18:1-8.

Katika mji fulani palikuwa na kadhi mmoja ambaye hakogopa mambo ambayo watu walimfikiria. Katika mji huo pia palikuwa na mwanamke ambaye mumewe alikuwa amekufa. Mwanamke huyu alikuwa na adui ambaye alimfanya kuwa na maisha magumu sana (yaani adui aliyemsumbua sana).

Alimwendea-endea kadhi yule akiitaka amsaidie. Alimtaka ampatie haki na kukomesha mateso ambayo adui wake alikuwa akimpatia. Kwa muda, yule kadhi alikataa kumsaidia.

Hakutaka kusumbuliwa na mwanamke huyu. Mwishowe, baada ya mwanamke huyu kumwendea-endea na kumwomba amsaidie, alikubali kumpatia haki ili asiweze kumwenda endea tena. Je, Yesu alikuwa akifundisha nini kwa hadithi hii?

Ikiwa kadhi yule dhalimu mwishowe alimpatia yule mwanamke haki kwa sababu alimwenda mara nyingi kumwomba, Mungu wetu mwenye haki na upendo atawapa

Walimwita, "Rafiki ya wenye dhambi." Kwetu sisi jina hili ni kufaraji. Yesu alidhihirisha kwamba yeye ni rafiki ya wenye dhambi kwa kuja ulimwenguni na kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Aendelea kudhihirisha kwamba yeye ni rafiki yetu kwa kukaa nasi kila siku, kwa kusema nasi kwa Biblia, na kutusikiliza tunapomwomba.

Siku moja, baada ya Yesu kuomba, mmojawapo wa wanafunzi wake alimwambia, "Bwana, tufundishe sisi kusali." Mwanafunzi huyu alijua kwamba mara kwa mara Yesu alizungumza na Baba yake. Yesu alijua vyema zaidi kuliko mtu mwingine ye yote jinsi ya kuzungumza na Mungu. Basi, Yesu akawafundisha wanafunzi sala inayojulikana kama "Sala ya Bwana." Sala hii ilikuwa mfano kwa wanafunzi, na kwetu sisi pia.

(Waongoze watoto kusali "Sala ya Bwana" Mathayo 6:9-13.)

Baada ya Yesu kuwapa wanafunzi wake mfano huu, sala, alikuwa bado ana mambo mengi ya kuwafundisha juu ya kusali. Alitumia mithali kuwasaidia watu kuelewa mambo aliyowataka wayasikie.

(Luka 11:5-13 ndiyo Maandiko ya hadithi ya kwanza kati ya hadithi hizi ambazo Yesu alisimulia ili kuwafundisha watu juu ya sala. Labda utataka kusoma hadithi hii kutoka kwa Biblia na kuifahamu.)

Kwa sababu ya joto jingi katika Uyahidi (Palestina), watu wengi walisafiri usiku. Yesu aliwaambia

wanafunzi wake, "Hebu tudhanie kwamba mgeni aliwasili usiku nyumbani kwako, na wewe ukawa huna cho chote cha kumlisha. Ukaondoka ukaenda kwa nyumba ya jirani yako, ukamweleza hali hiyo, na ukamwomba akukopeshe mikate mitatu. Na jirani akakujibu, "Nenda zako, usinitaabishe. Tumelala kitandani mimi na watoto wangu. Siwezi kuondoka nikupe kwa sababu ni kazi nyingi." Ikiwa uliendelea



kumwomba akusaidie, pengine mwisho wake aliondoka kitandani na kutimiza hitaji lake. Je, alikupa mikate hiyo kwa sababu ulikuwa rafiki yake, au kwa sababu alitaka uondoke umwache alale?"

Uliza: Je, Yesu alitaka kufundisha nini kwa hadithi hii?

Alitaka kuwaonyesha wanafunzi wake ya kwamba kama rafiki mchoyo akiweza kutimiza hitaji la rafikiye akimwomba, Mwenyezi Mungu aweza kutumainiwa kutimiza mengi zaidi kuhusu mahitaji yetu kwake. Wahitaji tu kumwomba Mungu kwa juhudi vitu vinavyolingana na mapenzi yake.

Yesu. Mtu huyu hakuwa Myahudi, bali alikuwa Msamaria. Alipoanguka kifufufudi miguuni pake Yesu, Yesu alimwambia, "Imani yako imekuoka."



Kristo aliponya miili ya wale watu wote kumi wenye ukoma. Lakini mmoja tu kati yao ndiye alirudi kumshukuru Yesu. Yesu alimpa tena zawadi nyingine ya ajabu mno. Alimponya ugonjwa wake wa dhambi. Yesu alikuwa na uwezo wa kuuponya ugonjwa wa ukoma na ugonjwa wa dhambi.

Uliza, Je, Yesu anao uwezo kama huo siku hizi?

Siku moja, Yesu alikuwa katika nyumba moja Kapernaumu akifundisha na kuwaponya watu wengi. Waandishi na Mafarisayo wengine walikuja, wakajaribu kuchunguza mafundisho yake ili waweze kumpata na hatia.

Katika mji huo kulikaa mtu mmoja ambaye alikuwa na ugonjwa wa kupooza. Mtu huyu hakuweza kusimama wala kutembea kwa sababu viungo vyake vyote vya mwili vilikuwa vimelegea.

Habari kwamba Yesu alikuwa Kapernaumu zilienea upesi. Muda kidogo yule mgonjwa akasikia habari hizo. Rafikize wanne walikuja kumbeba na kumpeleka kwa Yesu.

Bila shaka, walikuwa na furaha walipombeba kitandani mwake na kumpeleka katika nyumba ile alimokuwamo Yesu.

Bila shaka, waliudhika walipoi-karibia nyumba alimokuwamo Yesu na kuona kwamba hawawezi kumfikia Yesu. Mkutano wa watu ulikuwa mkubwa mno hata hakuna mtu aliyeweza kufika karibu na nyumba ile.

Je, watu hao wangepanya nini? Hawakuweza kurudi nyumbani bali waliamua kutenda jambo.

Katika siku hizo, dari za nyumba zilikuwa tambarare, na kulikuwa na ngazi ya kupandia juu. Kwa uangalifu, watu hao wanne walimbeba yule mgonjwa wakapanda juu ya dari ya nyumba ile ambamo



Yesu alikuwa akifundisha.

Walimwika chini, wakaanza kufanya tundu katika ile dari. Halafu wakamshusha mgonjwa na kitanda chake katikati mbele ya Yesu.

Yesu alipomwona mgonjwa huyu alisema, "Ee rafiki, umesamehewa dhambi zako." Alipokuwa akisema maneno haya ya msamaha, waandishi na Mafarisayo walijiuliza wao kwa wao, "Ni nani huyu asemaye maneno ya kukufuru? Hakuna mtu aliye na uwezo wa kusamehe dhambi. Ni Mungu pekee ndiye awezaye kufanya hivyo."

Uliza: Je, viongozi hawa wa kidini walikuwa na haki katika kusema kwamba Mungu pekee ndiye awezaye kusamehe dhambi?

Ndiyo! Lakini wao hawakutambua kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, na kwamba Yesu alikuwa na uwezo huu pia.

Yesu alijua fikira zao, akawauliza ni kwa nini walifikiria mambo kama hayo? Aliwaambia, "Lililo jepesi ni lipi? Kusema, 'Umesamehewa dhambi zako, au kusema, Ondoka, uende?'"

Bila kungojea wajibu swali lake, Yesu alimgeuka yule mwenye kupooza akasema, "Ondoka. Jitwike kitanda chako, ukaende zako nyumbani kwako." Mara hiyo aksimama, akajitwika kitanda chake, akaenda zake nyumbani kwake huku akimtukua Mungu.

KAZI YA KUFANYA

Kwa nini maisha ya yule mtu mwenye ukoma ya likuwa upweke mno? Hakuruhusiwa kuwa karibu na watu wengine.

Andika herufi "X" kwenye mstari ulio mbele ya jibu sawa la maswali yafuatayo.

Wale watu kumi wenye ukoma walikuwa wakiomba fedha.

Ndiyo X La
Wote kumi walimsihi Yesu awahurumie.

Ndiyo X La
Wote kumi waliponya ugonjwa wao wakarudi wote kumshukuru Yesu.

Ndiyo X La
Mmoja tu aliyerudi (kutoa shukrani) alikuwa Myahudi.

Ndiyo X La
Piga mstari chini ya maneno ambayo Yesu alimwambia yule kiwete kwanza.

"Dhambi zako zimesamehewa."

"Simama uende."

Piga mstari chini ya sababu Yesu aliyotoa kwa kumponya yule kiwete.

Ili wale wanaotazama wajue kwamba Yesu ana uwezo wakusamehe dhambi.

Ili kwamba yule kiwete awe mtumishi wa Yesu.

Sura ya Kumi

YESU AFUNDISHA JUU YA MAOMBI

MASOMO YA BIBLIA: Mathayo 6:9-13; Luka 11:5-13, 18:1-14

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Vitu vingi ni vya muhimu maishani mwa Mkristo na kitu kimoja ambacho ni cha muhimu sana kuliko zote ni ule wakati anaotumia Mkristo akizungumza na Mungu katika maombi. Maisha yetu ya kuomba yatusaidia kukua katika imani yetu na kuwa Wakristo imara. Mara nyingi Yesu alitumia umuhimu wa kuomba. Yeye mwenyewe alionba na akatiunyesha mfano.

Wakristo wengi huzungumza juu ya maombi. Labda wanafunzi wako husikia mambo mengi zaidi ya maombi shuleni au kanisani. Labda husikia watu wazima wakioambi. Je, wao wenyewe wanaomba kadiri gani? Je, wanajua uwezo ambao hupatikana na kila mmoja wetu kwa maombi? Na maombi yako je? ayategemea kadiri gani?

Unapofundisha, yafaa ukumbuke kusudi mbili. Kwanza, wewe kama mwalimu, inakupasa kuwasaidia wanafunzi wako kutambua ya kwamba Bwana atatutia moyo tupkee vitu vyake vyema kwa njia ya maombi. Kimoja kati ya vitu hivi vyema ni ushiriki wa kuwa karibu naye. Kusudi la pili ni kuwasaidia wanafunzi wako wakate shauri kuomba kila siku. Hizi ni hatua muhimu za kuwasaidia vijana kuishi maisha ya Mkristo. Yatupasa sisi

sote kujifunza somo hili linalofundisha kwamba Mungu anayo vitu vingi vyema ambayo anatoka kumpa kila mmoja wetu lakini sisi ndio hatumwombi. Tunakosa kupata baraka zake nyingi kwa sababu hatuombi kama inayotupasa. Somo hili la leo litatusaidia kujifunza kuomba kama inayotupasa kwa kufuata mfano hasa wa Yesu mwenyewe.

MAMBO YA KUKAZA

1. Twaweza kuwa na ushirika na Mungu tukitumia wakati mwingi katika maombi.

2. Yatupasa kuomba kwa juhudi hasa, kuomba bila kuchoka, na kuomba kwa unyenyekevu.

3. Ili tuweze kufanikiwa kwa maombi, ni lazima tuombe hasa, wala tusizungumze tu juu ya maombi.

KULIFUNDISHA SONO

(Soma Waeleso 1:2-3 wakati wa kufungua mafunzo ya darasa.)

Mwana wa Mungu anajulikana kwa majina mengi tofauti. Je, ni jina lipi ambalo lipo katika vifungu vya Maandiko vya Waeleso 1:2-3? (Bwana Yesu Kristo.) Mungu alimpa Mwanawe jina kuu katika ulimwengu wote, na alisema kwamba siku fulani, kila mmoja atamwinamia Bwana na kumwabadu.

Maadui wa Yesu walimpa jina ambalo lilikusudiwa kumwudhi.

Watie wanafunzi wako moyo kuwa macho na kuwa tayari kutumia nafasi zao kwa kazi ya Kikristo ambayo pengine watakuwa nayo juma lijalo.

Unapofunga somo hili kwa maombi, utahitaji kuomba ili Bwana awasaidie wewe na wanafunzi wako kutoa kadiri mnavyoweza kwa wana. Omba ili Bwana awaonyeshe nafasi zilizo, na kwambaazidi kuwapa nafasi nyingi zaidi za kumtumikia.

Piga mstari chini ya kifungu cha maneno kinachosema kile yule mtu alichofanya baada ya kuponywa na Yesu.

Alimwomba Yesu amponye mmojawapo wa rafiki zake aliyekuwa mgonjwa.

Alikitwaa kitanda chake, akaenda zake nyumbani akimtukuza Mungu.

Katika Luka 5:18 tafuta jinsi mgonjwa yule alivyochukuliwa na kupelekwa kwenye nyumba Yesu alimokuwa.

Alibebwa na rafiki zake wanne kitandani mwake. Kwa nini hawakumchukua kupitia mlangoni? Makutano ya watu walikuwa wengi zaidi.

Je, ni jinsi gani walivyomfikisha mgonjwa yule kwa Yesu?

Walimshusha katika lile tundu walilolifanya darini mpaka chini mbele ya Yesu.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Akasema, yasiyowezekana kwa wanadamu yawezekana kwa Mungu." Luka 18:27

Kuna mambo mengi ambayo hatuwezi kujifanyia sisi wenyewe. Mwanadamu hajapata dawa ya kuponya mgonjwa mengine na pengine hutaweza kamwe. Lakini Mungu anao uwezo wa kuponya kila ugonjwa ikiwa ana nia ya kufanya hivyo. Ni vigumu kwetu siku hizi kumponya mtu mwenye kupooza. Walakini, Yesu alisema tu, na yulemtu aliyekuwa na mgonjwa kwa

miaka mingi akainuka na kutembea. Kwa Mungu, jambo hilo liliwezekana.

Kuna ugonjwa mmoja ambao hatuwezi kuuponya sisi wenyewe. Ugonjwa huo ni dhambi. Mwanadamu hawezi kujiponya mwenyewe, au kujisamehe dhambi. Hili ni jambo lililowezekana kabisa kwa mwanadamu.

Lakini kwa sababu ya upendo mkuu alio nao Mungu kwa watu wote ndio maana yeye hutusamehe dhambi zetu. Mwanadamu hawezi, lakini Mungu aweza. Twahitaji kumtegemea Mungu kufanya mambo ambayo hatuwezi kuyafanya sisi wenyewe, kwa sababu ni Yeye tu mwenye uwezo huo.

WAKATI WA KUFUNGA

Uliza: Ni mambo yapi ambayo huwezi kujifanyia wewe mwenyewe, na ambayo kwayo wataka Mungu akusaidie?

Unapofunga somo, watie moyo wanafunzi wako ili wajifunze kutokana na hadithi hizi ya kwamba Yesu hana tu uwezo wa kuponya miili yetu peke yake, bali anao pia uwezo wa kuponya mioyo yetu. Anaweza kuyaponya mgonjwa na dhambi zetu. Walakini, ni lazima tuwe wale wasemao kwa Mungu, "Najua kuwa siwezi kufanya jambo hili mimi mwenyewe. Tafadhali, nifanyie."

Wakati wa maombi utahitaji kumwomba Mungu akusaidie wewe na wanafunzi wako kutambua unyonge wenu na kutegemea nguvu zake.

YESU AFUNUA UTUKUFU WAKE

MASOMO YA BIBLIA: Luka
9:28-43; Marko 9:14-29

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Kila siku watu hukwambia mambo ya kufanya. Hukwambia, "Fanya hivi." "Nenda pale." "Kaa hapa." "Nyamaza." Ni lazima tukate shauri kama tutaziti amri hizi ama la. Biblia inatwambia kwamba Yesu alitumuru kumpenda Mungu kwanza.

Pia inasema, "Mpende jirani yako kama nafi yako." Hizi ni amri tunazopewa kutoka kwa Mungu. Ni juu yetu kukata shauri kama tutaziti au la. Yafaa tuyasikilize maneno anayotwambia Yesu ili tuweze kumtii.

Waweza kuuliza swali hili, "Je, twamsikiaje Yesu?" Twamsikia Yesu kwa kusoma mambo anayotwambia katika Neno la Mungu. Wiki hii pia tutahitaji kuuliza swali, "Kwa nini nimsikilize Yesu?" Tutajibu swali hili kwa kuangalia hadithi mbili kutoka maisha ya Kristo. Hadithi hizo zinaweza kutusaidia kuona umuhimu wa kumsikiliza Yesu.

Kusudi la mafundisho yetu siku ya leo ni kuwafundisha wanafunzi ya kwamba Mungu ametuamuru kumsikiliza Mwanawe, na kwamba tunaweza kumsikiliza Yesu kwa Neno lake Mungu. Tokeo la somo hili liwe la kuwafanya wanafunzi wako watamani kumsikiliza Yesu akisema nao kwa Neno la Mungu.

MAMBO YA KUKAZA

1. Yatupasa kumsikiliza Yesu kwa sababu yeye ni Mwana wa Mungu, tena ana uwezo wa kupashana nasi ujumbe wa Mungu kuliko vile Musa na Eliya walivyoweza kupashana nasi.

2. Yatupasa kumsikiliza Yesu kwa sababu maneno yake yanawapa wale wanayoyamini uwezo wa kuishi maisha mapya.

3. Twaweza kumsikiliza Yesu akisema nasi Neno la Mungu.

KULIFUNDISHA SOMO

Yesu alijua kwamba muda mfulupi ataangikwa msalabani na kutoa maisha yake kwa ajili ya dhambi za watu wote ambao watamwamini kuwa yeye ni Mwokozi. Wanafunzi wake hawakujua ya kuwa Rafiki na Mwalimu wao atakufa kwa kifo kama hicho, ingawa Yesu alikuwa amekwisha kuwaambia. Maneno yake juu ya kufa na kufufuka katika wafu yalikuwa ya kuwashangaza sana wanafunzi wake.

Siku chache baada Yesu kuwaambia wanafunzi wake juu ya kifo chake, aliwachukua watatu kati ya wanafunzi hao wake, akapanda nao mlimani. Wanafunzi hawa walikuwa Petro, Yakobo na Yohana. Pengine ilikuwa wakati wa jioni ambapo Yesu alianza kupanda mlimani na wanafunzi wake hawa watatu. Walipofika juu ya mlima (kwenye kielele), pengine Yesu

Tunaweza kumhurumia mtu aliye na huzuni na kumfanya kuwa na furaha.

Kupanga jinsi ya kutumia nafasi hizi kunatugekea sisi. Tunaweza kuzidharau nafasi hizi, au kuona vibaya tunapozipoteza bure bila kuzitumia. Hata tunaweza kukosa kuzitambua kuwa ni nafasi tulizopewa na Mungu kwa utumishi wake. Walakini, siku moja, tutasimama mbele za Mungu kueleza mambo yote tuliyofanya kwa nafasi alizotupa.

Tu muhimu sana katika ufalme wa Mungu, na Mungu anategemea sisi kutimiza kazi yake. Tutoe kabisa maisha yetu yote kwa Mungu ili ayatumie katika njia yo yote anayotaka.

KAZI YA KUFANYA

Piga mistari chini ya majibu yaliyo sawa:

Kabaila alisafiri kwenda nchi ya mbali kutafuta mke.

Kabaila alimpa kila mtumwa wake almasi na johari kumweka wakati alipokuwa amcondoka.

Watumwa wake wawili walimpatia faida akawaluza.

Mtumwa wa tatu aliweka fedha aliyopewa na bwana yake kwa watao riba ili ajapo apate faida yake.

Kabaila aliwaadhibu watumwa wake wote watatu kwa mambo waliofanya.

Weka alama (X) katika mistari iliyo kando ya sentensi ambazo

tunaweza kutumia kuonyesha tabia za mtumwa yule wa tatu.

X Hakufanyia biashara fedha ile aliyopewa na bwana yake ili ampate faida.

Alifurahi kwa sababu alitenda haki.

X Aliadhibiwa kwa mambo aliyofanya.

Alijaribu kumlaumu bwana wake kwa mambo yaliyofanyika.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Nawaambia, kila aliye na kitu atapewa, bali yule asiye na kitu atayang'anywa hata alicho nacho." Luka 19:26

Mungu ametupa uwezo na akili hizi tulizo nazo. Alitupa vitu hivi kwa sababu fulani -- tuitumie kwa kazi ya ufalme wake. Anataka tuitumie katika kila nafasi. Tukivitumia, tutabarikiwa na kupewa mamlaka juu ya mambo makubwa zaidi. Tusipovitumia, Mungu atavipokonya kutoka kwetu kwa sababu havitakuwa na msada kwa mtu ye yote -- "yule asiye na kitu atayang'anywa hata alicho nacho."

WAKATI WA KUFUNGA

Pengine utapenda kuimba wimbo nambari 58 katika *Nyimbo za Sifa* usemao: "Yote Namtaolea Yesu."

Ukipenda, funga kwa kukaza jinsi kila mwanafunzi wako aliyvo muhimu katika kazi ya Bwana. Waambie, "Ninyi -- ni ninyi pekee yake -- mna uwezo na akili maalumu ambazo Mungu anaweza kutumia."

Baadaye uliza: Je, wafikiri kabaila alimtuza mtumwa huyu kwa tuzo chache kuliko yule wa kwanza kwa nini? Wafikiri mtumwa huyu aliwaza nini moyoni mwake? Kama ni wewe ungewaza nini? (Ngojeka wanafunzi wakupe majibu.)

(Mwisho waruhusu kabaila na mtumwa wa tatu kuzungumza.)
Baadaye uliza: Je, kabaila alimfikiri nini mtumwa huyu? (Waruhusu wanafunzi kutoa maoni yao juu ya mtumwa huyu.)

Watumwa wawili walimletea bwana wao faida. Mtumwa wa kwanza alifanya kazi kwa bidii sana akapata tuzo kubwa. Wa pili naye akafanya kazi kwa bidii akatuzwa. Lakini wa tatu hakufanya cho chote.

Mara nyingi sisi hufikiria sababu na udhuru wa kutoa wakati tunapofanya mambo ambayo hayatupasi kufanya, au tunapokosa kutimiza wajibu muhimu ambao unatupasa kufanya -- kama kuwaambia watu habari za Yesu au kuwasaidia wengine katika shida zao.

Kabaila alionyesha wazo gani? Je, kama mtu alikupa kitu fulani umfanyie, kisha wewe hukufanya hivyo, mtu huyo alikufanyaje?

Labda mtumwa wa tatu alificha fedha yake kwa sababu hakujiamini yeye mwenyewe. Aliogopa kwamba pengine angepoteza fedha ile.

Au pengine alifikiri kwamba hapakuwa na jaha ya kufanya juhudi ya kumletea bwana wake faida kwa sababu alikuwa "mtu mgumu na angetaka faida ya fedha aliyompa."

Ilimpasa mtumwa yule kutambua kwamba bwana yake alimwamini sana kwa kumwachia fedha.

Bwana hakumwambia yeye wala watumwa wale wengine jambo la kufanyia fedha zile. Alinyamaza tu apate kuona mambo ambayo wao wenyewe wangeamua kufanya.

Watumwa wawili wa kwanza walifanya bidii wakapata faida. Matendo yao yaliwaitea vyeo vya uliwalii juu ya miji kumi na mitano. Wajibu wao katika mambo madogo kuliwaitea tuzo na mamlaka juu ya mambo makubwa zaidi.

Mungu hututendea sawa na vile kabaila alivyowatendea watumwa wake. Mara nyingi Mungu hatuambii hasa jambo la kumfanyia. Yeye hutupa tu nafasi za utumishi na kungojea kuona mambo tutakayotenda kwa nafasi hizo.

Kwa mfano, tunaweza kumwona mtu aliye katika hali ya upweke, ambaye tunaweza kuzungumza na kushiriki naye habari za Yesu.



aliomba pamoja nao kwa muda kidogo. Lakini baada ya wakati mchache rafikize walilemewa na usingizi, wakalala. Bila shaka, kule kupanda mlimani kuliwafanya kuwa wachovu. Wanafunzi hao walipokuwa wamelala, Yesu aliendelea kusali peke yake.

Yesu alipokuwa akiomba, jambo la ajabu lilifanyika. Uso wake uling'aa kama jua, na mavazi yake yakawa meupe mno. Kwa ghafla pakatokea watu wawili wakizungumza na Yesu.



Uliza: Watu hawa walikuwa akina nani? (Musa na Eliya)

Watu hawa wa Agano la Kale walikuwa wameshakaa mbinguni miaka mingi sana. Katika siku za Yesu watu waliwakumbuka Musa na Eliya kwa heshima kuu. Viongozi hawa wawili walikuwa wamecipa Israeli ujumbe wa Mungu. Na sasa walikuwa wamerejea ulimwenguni

kuzungumza na Yesu kwa muda kidogo tu juu ya kifo chake kilicho wadia.

Ni jambo hili la muhimu ndilo liliwarudisha Musa na Eliya kuzungumzana hapa ulimwenguni. Kuzaliwa, kifo na ufuo wake Yesu yalikuwa, na hata sasa yangali, mambo muhimu zaidi ulimwenguni.

Hebu tudhanie kwamba watu hao wawili (Musa na Eliya) wamesema. Pengine wanasema hivi: "Yesu, wengine tulikutazamia kuja wakati tulipoishi ulimwenguni. Tuliamini kwamba utakuja siku fulani. Sasa uko ulimwenguni kuwaonyesha watu jinsi Mungu alivyo. Lakini, watu wengine havataamini ya kwamba u Mwana wa Mungu."

Utateseka mikononi mwa wale wanaokuchukia, ingawa wewe wawapenda. Watakuua kama mhalifu, ingawa hukutenda dhambi kamwe. Hii itadhihirisha milele kwamba Mungu apokea sadaka yako halisi kwa ajili ya dhambi. Baba yako, Mungu, atakutukuza. Siku fulani kila ulimi au kinywa kitakiri ya kuwa wewe ndiye Bwana."

Musa na Eliya walipokuwa pamoja na Yesu, wanafunzi waliamka. Waliona utukufu wa Yesu, wakawatambua wale watu wawili waliokuwa pamoja naye kuwa ni Musa na Eliya.

Wanafunzi waliona kwamba Musa na Eliya walikuwa wakijitayarisha kuondoka. Petro akatoa dokezo kwamba, Bwana mkubwa, ni vizuri

sisi kuwapo hapa. Tufanye vibanda vitatu; kimoja chako wewe, na kimoja cha Musa, na kimona cha Eliya."

Petro alipokuwa akisema, lilitokea wingu ikawaia uvuli. Sauti kutoka katika wingu hilo ikasema nao. (Mwambie mwanafunzi mmoja asome mambo yaliyosemwa na sauti hiyo. Mambo hayo yapatikana katika Luka 9:35, nayo ndiyo kifungu chetu cha leo.)

Mungu ndiye aliyekuwa akisema na alikuwa akiwafunulia wanafunzi hao ya kwamba Yesu ni Mwanawe. Pia, Mungu alikuwa akiwaamuru kusikiliza na kutii kila kitu Yesu atachosema. Yesu alisitahili hesima zaidi kuliko mtu ye yote; kuliko vile Petro alivyotaka kuwapa Musa na Eliya!

Wanafunzi walipoinua macho yao juu, Musa na Eliya walikuwa wanekwisha kuondoka na Yesu alikuwa anasimama peke yake. Alivaambia wanafunzi hao kuto-mwambia mtu ye yote hayo walioyaoona mpaka atakapofutuka katika wafu. (Labda utahitaji kusoma zaidi juu ya mambo haya kama yanavyopatikana katika Mathayo 17:8-9)

Wakati ulifika kwa Yesu na wanafunzi wake kushuka mlimani. Walipofika nchini ya mlima, walikuta mkutano mkubwa wa watu ambao walikuwa wanekuja kukutana na Yesu. Na mmoja katika mkutano huo alipaza sauti, akimwita Yesu.

Yesu alipomsikia mtu yuyo alimhurumia. Mtu huyo alimwambia



Yesu kwamba alikuwa na mwana kijana ambaye alikuwa mgonjwa. Mwana huyo wakati fulani alianguka-anguka chini na kushikwa na kifafa. Baba huyo alifikiri kwamba pepo ndiye humpagaa na kumfanya kuanguka-anguka. Alikwisha waomba wanafunzi wa Yesu hapo kitambo kumponya mwanawe huyo lakini walishindwa. Sasa alikuja kwa Yesu kumwomba msada wake.

Baada ya mtu huyo kumwambia Yesu maneno haya yote, Yesu alimwambia akanletee mwanawe. Kwa upendo mkuu, Yesu alimponya mwanawe huyo. Baadaye wanafunzi wakamwuliza Yesu kwa nini wao hawakuweza kumponya. Yesu akawajibu, akawambia, "Imani yenu ni chache. Pepo kama huyu hawezi kutoka kwa neno lo lote, isipokuwa kwa kuomba." Wanafunzi wamokuwa wakijaribu kumfanya Yesu kazi bila kuwa na uwezo wake.

Kwa nini walifikiri kwamba Mungu ametupa masimulizi haya ya uwezo na utukufu wa Yesu? Ni kwa sababu Mungu atwambia kwamba Yesu ni Mwanawe, na kwamba tumsikilize na kufanya yale anayosasema.

Je, ni jinsi gani waweza kujua mambo ambayo Mungu ataka

Mchezo huu unafuata sehemu fupi yenye maelezo chini ya "Kulifundisha Somo." Hakikisha kwamba sehemu hiyo imesomwa ili watoto waweze kuwa na tamaa ya kushiriki.

Je, unapendelewa na kumsaidia kila kijana na kumfanya kujifunisa nguvu na uwezo wake? Unawafikiriaje vijana wako?

Watu wazima na vijana wakati mwingine hufikiri kwamba hawana jambo lo lote la kushiriki na wengine. Unafikiriye wewe mwenyewe? Ni jambo gani unaloweza kushiriki na wanafunzi darasani mwako ambalo linaweza kumfanya Mungu kutukuzwa? Kila mtu ni mwema machoni pa Mungu kwa sababu yeye ndiye aliyetumba.

MAMBO YA KUKAZA

1. Mungu alimpa kila mmoja wetu uwezo na akili ambazo anatumia kutumia kwa njia kamili.

2. Watumwa wale watatu walipewa fedha, wakaulizwa kueleza jinsi walivyotumia fedha zile.

3. Watumwa waliotumia fedha zao kwa njia nzuri walifurahi na waliuzwa kwa kazi yao njema waliyoifanya. Yule mtumwa ambaye hakutumia fedha yake aliyopewa alihuzunika na hakuukuza kitu cho chote.

KULIFUNDISHA SOMO

Sema: Hebu tudhanie kwamba tunatembea karibu na Yerusalemu. Kwamba tunapokaribia mlima tunamwona Yesu na wanafunzi wake ambao wanekusanyika kwake.

Kwamba tunapowaendea karibu tunamsikia esu akianza kuzunguma na wanafunzi hao wake kwa funbo ambalo liwasisaidia kuelewa barabara mambo anayotaka kuwaambia.

Yesu atatusimulia hadithi juu ya kabaila na watumwa wake watatu ambao aliwapa fedha wakati aliposafiri kwenda nchi ya mbali. Unaposikiliza funbo hili, fikiri ni kwa nini Yesu aliwasimulia wanafunzi wake hadithi hiyo.

Uliza: Je, mipata kuambiwa kutunza kitu fulani wakati mwenyewe alipokuwa hayupo? Je, kulifanyika nini? Mlifurahi au mlihuzunika wakati mwenye kitu hicho aliporudi na kukitaka? (Waruhusu wanafunzi wako kujibu maswali hayo.)

Sema: Sasa tutaanza mchezo wetu wa kuiga hadithi hii. (Kabaila ndiye atakayeanza kusoma sehemu yake katika kitabu cha mwanafunzi.)

Uliza: Kwa nini walifikiri kabaila aliwapa watumwa wake fedha sawa kumwekea? Utiwaza nini kama mtu akikupa wewe fedha nyingi kama hizo kumwekea? Utafanya nini?



Waruhusu kabaila na mtumwa wa kwanza kuzunguma.) Baadaye uliza: Je, mwalifikiri kabaila alimtuza mtumwa huyu kwa njia hiyo aliyofanya kwa nini? (Wape wanafunzi nafasi wajibu.) (Kisha waruhusu kabaila na mtumwa wa pili kuzunguma.)

YESU ASIMULIA HADITHI JUU YA WATUMWA WAAMINIFU

MASOMO YA BIBLIA: Luka 19:11-22

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Mungu alimpa kila mmoja wetu uwezo na akili hizi tulizo nazo.

Alitupa vitu hivi tuweze kuvitumia utukufu na heshima yake. Wakati mwingine hatutumii vitu hivi bali tunavificha. Tunapofanya hivyo, havihusaidii sisi wala havimsaidii mtu mwingine ye yote.

Kwa mfano, mtaalamu wa sayansi anaweza kuvumbua dawa ya kuponya ugonjwa fulani uwaowaua watu sana. Asipowaonyesha madaktari uvumbuzi huo wake, ugonjwa ule hautaweza kuponywa bali utaendelea kuwaua watu wengi. Uvumbuzi huo usipotumiwa hautakuwa na msaada kwa mtu ye yote.

Labda wengi wetu hawataweza kamwe kuwa wataalamu wa sayansi wanaovumbua dawa za kuponya magonjwa. Ingawaje, sisi kama Wakristo tuna dawa ya kuponya ulimwengu, Yesu Kristo. Ni juu yetu kushiriki habari za Yesu na wengine kuliko kuficha mambo hayo ambayo yanatupasa kuwambia watu. Siku moja tutasimama mbele zake Mungu na kueleza mambo uliyokwisha kuyafanya kwa uwezo na akili alizotupa.

Somo letu la leo linasimulia hadithi juu ya watumwa watatu

ambao walimweleza bwana wao mambo waliyofanyia fedha alizowapa. Watumwahawa watatu walipewa fedha sawa na bwana wao. Wakati bwana wao aliporudi, aliwauliza kueleza mambao waliyofanyia fedha zile.

Tutatumia mchezo katika somo hili kusimulia hadithi juu ya kabaila na watumwa wake watatu. Labda utataka kuwatia moyo wanafunzi wako kushiriki katika sehemu za mchezo huu. Itakuwa muhimu kwako kutumia kitabu cha mwanfunzi pamoja na chako. Kuna sehemu tano katika mazungumzo ya mchezo huu. Chagua mtoto mmoja kuwa kabaila, wengine watatu kuwa watumwa wale watatu, na wewe kuwaongoza.

Nyote mtakuwa watu watano. Wakati huu ndio unaofaa hasa kuwatumia wanafunzi wako ambao mara kwa mara hawashiriki katika jambo lo lote darasani. Mara nyingi watoto hufikiri ya kwamba hawana darasani au la kushiriki na ulimwengu. Hii ndiyo nafasi nzuri sana kwako kukaza kwamba Mungu anawapenda na kuwapokea watu wote.

Wakati unapoanza kuwachagua wanafunzi wale watakaoshiriki katika mchezo huu, wachague wale wenye haya na wale wanaohitaji kutiwa moyo.

kukuambia? Mwana wa Mungu ndiye wa pekee ambaye aweza kukuonyesha Mungu, na ambaye maneno yake yana uwezo wa kukupa uzima na furaha. Je, unataka kumpa Kristo nafasi ya kwanza maishani mwako kwa kumsikiliza akikusemea kwa njia ya Biblia? Ikiwa kweli wataka kumsikiliza, atasema nawe katika roho yako.

KAZI YA KUFANYA

Siku moja Yesu aliwachukua wanafunzi wake watatu pamoja naye kuwaonyesha tukio ambalo hawangeweza kusahau. Kata neno lisilo sawa katika vifungu vifuatavyo na uandike neno lililo sahihi katika nafasi zilizoachwa.

kusali Yesu alipanda mlimani ~~kufata~~.

Yakobo Yesu aliwachukua Petro, ~~Andrea~~ na Yohana pamoja naye.

Meupe Yesu alipokuwa mlimani sura yake ilibadilika na mavazi yake yakawa ~~metundatu~~.

Andika herufi "X" katika mstari mbele ya vifungu vilivyo sawa.

X Kijana alikuwa na pepo mchafu.

Baba aliendelea kumpeleka mwanawe kwa madaktari.

X Yule baba alikuwa amempeleka mwanawe kwa wanafunzi wa Yesu.

X Wanafunzi wa Yesu hawakuweza kumtoa yule pepo mchafu.

Wanafunzi hawakujaribu kumsaidia yule kijana.

Wanafunzi wa Yesu hawakuweza kumsaidia yule kijana kwa sababu hawakuwa na imani ya kutosha.

Yesu alimwambia yule baba amfanyeje mtoto?

Amlete mtoto wake kwake.

Yesu alimfanyia nini yule mtoto?

Alimponya na kumpa baba yake.

Hii iliwafanya watu wote kuonaje?

Kushangaa kwa utukufu wa Mungu.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Sauti ikatoka katika wingu, ikisema, Huyu ni Mwanangu, mteule wangu, msikieni yeye. Luka 9:35

Mungu mwenyewe ndiye aliye-kuwa akisema na wanafunzi hawa! Alikuwa akiwaambia kwamba Yesu, ambaye walikuwa wakisafiri naye katika Uyahudi (Palestina) ni Mwanawe. Pia Mungu aliwaamuru kusikia na kutii mambo yote ambayo Yesu aliwaambia wafanye.

Mungu hajachagua kusema na watu wengi katika njia hii. Kuna Maandiko machache katika Biblia kuhusu wakati ambapo watu walisikia sauti hasa ya Mungu. Ni vigumu kwetu kufikiri jinsi wanafunzi hawa walivyoshangaa! Mungu alikuwa akisema nao hasa!

Mara kwa mara twasahau kujua kwamba Mungu husema nasi siku hizi

pia. Amekwisha chagua njia tofauti za kusema nasi. Twaweza kumsikia akisema nasi kwa Biblia ambayo ni Neno lake. Kuna mambo mengi ambayo aweza kutuambia ikiwa tunasoma na kufuata mambo anayotupangia.

WAKATI WA KUFUNGA

Uliza: Ni kwa nini wafikiri kwamba Mungu amekupa masimulizi ya uwezo na utukufu wa Yesu.

Kwa nini wanafunzi hawakulifanya jambo hili kuwa siri hata baada ya Yesu kufufuka katika wafu?

(Wape wanafunzi wako wakati wa kuzungumza.)

Hadithi hii ni muhimu kwa sababu kwayo, Mungu mwenyewe akwambia ya kwamba Yesu ni Mwanawe mpendwa, na kwamba umsikilize na kufanya mambo yale anayokwambia.

Mwana wa Mungu ndiye wa pekee anayeweza kukuonyesha au kukuongoza kwake Mungu. Je, wataka kumpa nafasi ya kwanza maishani mwako kwa kumsikiliza akisema nawe kwa Biblia? Ikiwa kweli wataka kumsikiliza, atazungumza nawe rohani mwako.

Unapofunga somo hili kwa maombi, omba ili kwamba tamaa ya moyo wako iwe ya kusikiliza mambo Mungu anayokuambia **WEWE** kwa kusoma Biblia yako na kwa maombi.

ndiyo fikira ya ajabu kwetu sote! Mungu atupenda sisi sote!

Itakuwa jambo la huzuni ikiwa kuna mmoja kati ya wanafunzi wako asiyejua upendo huu wa ajabu. Omba ili kwamba ukweli wa Neno lake Mungu upenye na kuingia katika mawazo ya wanafunzi wako. Omba ili kwamba Mungu awape ufahamu watu wale wapoteao dhambiini wajue kwamba anawatafuta.

Yesu alisimulia hadithi ya mwanamke mmoja aliyepoteza kitu. Jaza nafasi zilizo katika hadithi iliyo hapo chini juu ya mwanamke huyo.

Mwanamke mmoja alikuwa na shilingi 10. Lakini aligundua kwamba amepoteza 1 kati ya shilingi hizo. Kwa haraka aliwasha taa na kuitafuta. lipoipata, alikwenda kwa nyumba ya jirani yake. Akamwambia, "Furahi nami, kwa kuwa nimeipata shilingi iliyonipotea."

Piga mstari kutoka kwa picha ya mwana mpotevu hadi kwa kila sentensi ya kweli inayosimulia habari zake.

A l i k a a nyumbani na kufanya kazi shambani.

A l i t u m i a fedha zake kwa mambo ya uasherati.

Alikuwa na chakula kingi cha kula.

Alipata kazi ya kulisha nguruwe.

A l i k u l a c h a k u l a a l i c h o w a l i s h a nguruwe.

A l i k a t a

shauri kurudi nyumbani kwa babaye.

Hakusikitika kwamba alimtenda Mungu dhambi pamoja na baba yake.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea." Luka 19:10

Kama ukipoteza fedha zako, hata kama ni kidogo, utafanya nini?

Utazitafuta mpaka uzipate. Au kama ukipoteza ndugu au dada mwituni au katika njia za mji mkubwa, utamtafuta mpaka umpate. Wakati wo wote tunapopoteza kitu, tunakitafuta mara moja. Kadhalika, Mungu pia ni hivyo.

Mungu anawakaribisha watu wote wanaopotea dhambi kutubu dhambi zao na kumrudia yeye. Kila wakati mwenye dhambi anapotubu na kumrudia Mungu, malaika wote wa mbinguni hufurahi kwa furaha kubwa. Ni jambo jema na la ajabu kujua kwamba sisi tu muhimu sana kwa Mungu.

KULIFUNGA SOMO

Hadithi kuhusu vile Mungu anavyowatafuta watu waliopotea dhambi na kuwarudisha kwake ndiyo njia nzuri ya kuwaonyesha watoto upendo mkuu ambao Mungu anao kwa watu wote, na hasa kwao.

Hadithi ya mwana yule aliyetangatanga na kujiingiza katika maisha ya uasherati, na aliyesamehewa na kukubaliwa tena nyumbani ni hadithi ya upendo wa Mungu kwa wenye dhambi.

Mungu atupenda bila kutazama dhambi zetu. Aweza kujifanya maisha yetu maovu kuwa mema. Hii

YESU AWATUMA WASAIDIZI SABINI

MASOMO YA BIBLIA: Luka 10:1-24

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Hakuna furaha kuu zaidi kwa Mkristo kuliko kumshiriki Kristo na wengine. Walakini, wakati mwingine hili ndilo jambo moja ambalo ni vigumu kuwaongoza Wakristo kufanya. Mara kwa mara tunaogopa kushiriki imani yetu na wengine ambao hawaamini. Somo letu siku hii latuambia jinsi Yesu alivyowatuma wanafunzi wake sabini kwenda kueneza Habari Njema ya wokovu.

Tunapotumwa kwa ujumbe fulani, au kuulizwa kumfanyia mtu fulani jambo, tunapewa maagizo au maongizi ya kufuata. Wasaidizi hawa sabini walipewa maagizo yenye maelezo kamili kwa kazi yao, na somo la leo la tuambia juu ya maagizo hayo.

Namna ya somo letu la leo ni tofauti na ya masomo mengine. Tunatumia mchezo ili kusimulia hadithi ya wanafunzi hawa sabini.

Tafadhali, watic moyo wanafunzi wako ili washiriki katika mchezo wa somo hili. Kuna watu wawili tu katika mazungumzo haya. Itakuwa nafasi nzuri kuwaruhusu wawili kati ya wanafunzi wako ambao hujiunga mara chache katika mazungumzo ya masomo kushiriki katika mchezo huo.

Mara nyingi watoto ambao ni wakimya wakati wa somo, labda

watapenda kusema wakitiwa moyo wa kufanya hivyo. Hii ndiyo itakayokuwa nafasi inayowapasa kushiriki katika mchezo darasani. Unapowachagua wale ambao watashiriki, kumbuka mambo haya.


Mchezo wenyewe unafanywa kwa swali kwanza, halafu jibu. "Msaada wa mwalimu" utakuwa maelezo zaidi juu ya kila swali na jibu lake, na labda utataka kushiriki mambo haya na wanafunzi.

Mara kwa mara kusudi letu huwa ni kubadilisha matendo ya wanafunzi wetu wakati tunapowafundisha. Tusisahau kukumbuka ya kwamba nia ya mwanafunzi ndiyo muhimu pia. Njia yake juu ya wokovu ni ya maana sana. Kusudi lako wiki hii litakuwa ni la kuwasaidia wanafunzi wako waonyeshe furaha kwa wokovu wao.

Je, wafurahi kumpa Kristo nafasi ya kwanza maishani mwako? Furaha hii ni ya kuenezwa!

MIAMBO YA KUKAZA

1. Yesu awatuma wanafunzi sabini ili kuwatayarisha watu kwa mafundisho yake.
2. Wanafunzi hao walirudi wakifurahia miujiza waliyokwisha kufanya.
3. Walipata furaha katika kushiriki Habari Njema na wengine.



RULIFUNDISHA SOMO

Sema: Hebu tudhanie kwamba tuko kati ya marafiki maalumu wa Yesu.

Yesu atuliza tuje tukutanie pamoja. Na tunapokutanika pamoja tunashangaa ni kwa nini Yesu alitua katika mkutano huu. Ataka kutambua nini? Anayo kazi kwa sisi kufanya? Hebu tusikilize ile jambo ambalo Yesu amwambia mmoja wetu.

(Wakati huu waambie wanafunzi wako wawili uliokwisha wachagua wasome sehemu muhimu ya mchezo. Halafu kuwa na wakati wa mazungumzo ili mzungumze juu ya kila mojawapo ya maongozi ambayo Yesu alitoa kama jibu la maswali aliyoulizwa. Mazungumzo yenu yawe hivi.)

1. Kwa nini unatuma?

Yesu alisema ya kwamba watu katika miji na vijiji vya karibu walikuwa kama mavuno mengi ambayo yako tayari kuvunwa. Wanafunzi wale sabini walitumwa kwenda kuvuna mavuno haya.

Je, unewahi kuwaona wafanya kazi kondeni wakati wa mavuno? Ni lazima wavune hayo wakati unaofaa ama mbegu zitaharibika.

Yesu alikuwa akionya kwamba watu watapotea wasipopelekewa Injili wakati unaofaa. Ni jambo la kuhuzunisha kwamba kuna tu watenda kazi wachache wa Mungu. Na hii ndiyo sababu Yesu aliwaambia wanafunzi wale sabini waombe ili

Bwana apeleke watenda kazi wengi katika makonde yake.

2. Tuchukue nini katika safari yetu?

Yesu aliwaambia wanafunzi hawa kutochukua fedha zo zote katika mikanda yao ambayo ilikuwa kawaida yao kubebeka fedha. Wala hawakurubusiwa kuchukua mkoba wa kubebeka vyombo vyao kwa safari. Pia walipewa maagizo kwamba wasichukue jozi la viatu vingine isipokuwa viatu waliyovaa. Maagizo haya yalikuwa ni ya ajabu kwa watu ambao walikuwa karibu kuanza safari yao.

3. Tuwaambie nini wale tunaokutana nao njiani?

Tabia nyingine za watu wa Agano Jipya zilifanana na tabia za Kiafrika. Watu walipokutana njiani, hawakumuana tu kwa kusema "Habari ya asubuhi!" au "U hai gani?" Walianza kuulizana hali yao na ya kila mmoja katika jamaa zao. Kuamkuna huko kulichukua wakati mrefu sana.

Yesu alitaka watu hawa wafahamu kwamba walikuwa katika safari muhimu ya kufanya kazi ya maana sana. Hawakuwa na wakati mwingi wa kutumia wakamkuana. Ilikuwa lazima wavunje desturi hizo zao ili waweze kutimiza kazi hii.

4. Tuseme nini tunapowasili?

Yesu aliwaambia watu hawa kwamba wanapofika katika miji fulani, waende katika nyumba moja na kusema, "Amani iwemo nyumbani

Babaye alisema, "Mwanangu alikuwa amepotea na sasa ameonekana."

Wakati wa karamu, ndugu mkubwa alikuja kutoka shambani alikokuwa akifanya kazi. Alisikia sauti ya wimbo, akawauliza watumwa jambo lililokuwa likifanyika nyumbani. Watumwa walipomweleza yale mambo, alikasirika sana. Hakutaka kuingia nyumbani. Babaye alitoka nje, akamsihi aingie ndani, lakini yeye alisema, "Tazama, mimi nimekutumikia miaka mingapi hii, wala sijakosa amri yako wakati wote, lakini hujanipa mimi mwana-mbuzi, nifanye furaha na rafiki zangu. Lakini, alipokuja huyu mwana wako aliyekula vitu vyako pamoja na makahaba, nemmchinja yeye ndama aliyenona."

Babaye alijaribu kumweleza ya kwamba hakuwa anajaribu kumtaza mwanawe huyo aliyepotea kwa ajili ya dhambi zake, bali alikuwa akijaribu kuonyesha kwamba alikuwa na furaha kuu kwa kumpata mwanawe huyo tena. Ndugu huyu mkubwa alikuwa na kijicho, na hakuweza kuelewa maana hii.

Katika hadithi hii, ni nani anayesimama badala ya mwenye dhambi? Ndiyo, mwana yule aliycondoka nyumbani kwenda nchi ya mbali. Ni nani aliyesimama badala ya Mungu? Ndiyo, ni baba yao.

Yesu alitaka Mafarisayo na waandishi wajifunze nini kutokana na hadithi hizi? (Kwamba yeye huwaharumia wenye kupotea dhambiini)

Mungu ni kama yule mchungaji, yule mwanamke, na yule baba aliyemkaribisha mwanawe aliyepotea nyumbani. Kama vile baba aliyoyokimbia kwenda kukumbatia mwanawe aliyevaa matambaa, viyoo hivyo Mungu apenda kukuchukua kama ulivyo na kukufanya kuwa wake. Yule mwana aliondoka nyumbani labda alifikiri, "Hakuna maana. Baba hatanipokea tena kwa sababu nikuwa mwovu sana."

Lakini, Bwana Yesu alikuja kukutafuta na kukokoa. Alikuwa na akafutika tena ili kukuleta kwa Baba yake aliye mbinguni. Je, ungependa Bwana Yesu kukutaribisha tena katika jamii yake? Mwaambie sasa. Atakutaribisha.

KAZI YA KUFANYA



Mtu aliye picha hii anatafuta kitu. Yeye ni mchungaji ambaye alipoteza kitu. Jibu maswali


yafuatayo juu ya kile kitu alichopoteza mchungaji huyu.

Mchungaji huyu alikuwa na kondoo wangapi? 100

Wangapi walipotea? mmoja.

Alipompata kondoo huyo aliyepotea, alimchukuje nyumbani? Alimbeba mabegani.

Mchungaji huyu alifurahi pamoja na akina nani? rafiki zake na jirani zake.



mwana huyo alikuwa akifikiri nini? Wafikiri kwamba alikuwa akipanga kwenda katika mji mkubwa?

Labda alifikiria kwenda huko akiwa na fedha nyingi na kutofanya kazi.

Mara tu baada ya kupokea fedha zake, mwana huyo alikusanya vyombo vyake, akaanza safari yake. Alipofika huko alikodhamiria kwenda, yaani, nchi ya mbali, alitumia fedha zake kwa upumbavu mno.

Labda alikuwa na furaha wakati fedha zake zilikuwa hazijaisha. Na baada ya fedha zake kwisha njaa kuu iliingia nchi ile. Chakula kikawa kichache sana na matajiri tu ndio waliokuwa na chakula cha kutosha. Mwana huyo alianza kusikia njaa. Ilimbidi kujaribu kutafuta kazi. Lakini ilikuwa shida kupata kazi.

Mwishowe alipata kazi ya kuwalisha nguruwe. Twajua ya kwamba hakupokea mshahara mzuri kwa kazi hii kwa hivyo alishikwa na njaa mno hata akatamani kula chakula walichokula nguruwe.

Wadhani sasa alifikiri nini? Labda alifikiri hivi: "Ni nani anayejali kwamba nina njaa? Ni nani anayejali kwamba ninavaa atambara badala ya kuvaa nguo nzuri nilizokuwa nazo? Kama ningaliweka fedha ningalikuwa na shamba. Sasa mimi ni mtumwa tu. Nifanye nini? Nirudi nyumbani?"

Huu ulikuwa uamuzi mgumu sana kwake kufanya. Jirani wangemfikiri nini wamwonapo akitembea njiani kwenda nyumbani? Angeonekana maskini na mwenye njaa. Ndonguye mkubwa angemtendaje? Na jambo muhimu mno ni kwamba babaye angesemaje? Baba yake alikwisha kumfanyia yote yaliyompasa mtu kumfanyia mwanawe. Alikwisha kumpa urithi wake wote.

Kisha mwana huyo aliwakumbuka watumwa wa baba yake. Watumwa hao walipata vyakula vingi vyema. Basi kwa nini ateseke hivi na hali kulikuwa na vyakula vingi nyumbani mwa baba yake? Labda babaye angempatia kazi kama mtumwa wake, na bila shaka angepata chakula.

Alianza safari ndefu ya kurudi nyumbani kwao. Safari hii ilionekana ndefu sana kwake wakati huu. Alipokuwa njiani, aliwaza moyoni mwake juu ya jambo babaye angesema.

Mara, alimwona mtu akikimbia kujia kumlaki. Mtu huyo alikuwa ni baba yake! Babaye huyo alimkumbatia na kumbusu. Alikuwa akimtazamia mwanawe huyo na kutumaini ya kwamba siku moja atarudi.

Mwana huyo akasema, "Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena." Lakini kabla hajasema mengi, baba yake aliamuru vazi lililo bora liletwe ili avikwe, na pete ative kidoleni, na viatu avalishwe. Ndama alichinjwa na karamu ikaandaliwa.

humu." Ikiwa watu wa nyumba hiyo wawakaribisha wakae humo. Aliwaambia wasihamehame kutoka nyumba hii kwenda nyumba hii, wakila huku na huku. Yesu alijua kwamba kama wanafunzi wake watapokea makaribisho hayo yote, hawatakuwa na wakati wa kufanya kazi iliyowapeleka.

5. Tufanye kazi gani?

Yesu aliwapa wanafunzi hao sabini uwezo wa kuwaponya wagonjwa katika miji iliyowakaribisha. Pia aliwapa maagizo maalum juu ya mambo ya kuwaambia watu. Watu hawa walitumwa kuwaambia watu wajisikitishe kwa ajili ya dhambi zao. Walidhamiriwa kumtayarishia Bwana njia na kuwaambia watu kuwa ufalme wa Mungu ulikuwa umekaribia.

6. Tufanye nini tusipokaribishwa?

Yesu aliwaamuru wanafunzi hao kwamba, kama hawawezi kupata nyumba ya kuwakaribisha katika mji watakaolingia, wasimame katika mlango wa mji huo na kuyakung'uta mavumbi ya miguu yao na kuondoka. Hii itakuwa funzo kwa watu wa mji huo na ishara kwamba wanafunzi hao wamekwisha kutimiza wajibu wao wa kujaribu kuhubiri ujumbe wa Yesu. Hawakuhesabiwa hatia kwa watu waliokataa kuwasikiliza. Bwana Mungu hawashurutishi watu kulipokea Neno lake.

Hata siku hizi, twaweza kulisikiliza Neno lake na kutii, au twaweza kukataa kupokea vitu vyema ambavyo Yesu ataka kutupa.

Wanafunzi hao sabini ambao Yesu aliwatuma walikuwa wenye furaha nyingi waliporudi. Walikuwa wakintumikia Yesu. Walikuwa wamegundua kwamba waliweza hata kutawala pepo wachafu wakati waliposema nao katika jina la Bwana. Walifurahia uwezo huu.

Wanafunzi hao sabini walipata furaha katika kumtumikia Yesu na katika kuona miujiza, Je, na wewe wapata furaha katika njia hii? Je, umepata kuwa na furaha katika kumfanyia Yesu jambo fulani? Hii ndiyo furaha ambayo Yesu ataka kutupa, na mambo yanayotupasa kufanya ili tuweze kupata furaha hii ni kumshiriki Yesu na watu wengine.

KAZI YA KUFANYA

Yesu aliwatuma wasaidizi wake kwenda vijijini kumtangulia. Alisema ya kwamba watu ambao wasaidizi wake waliwatembelea walikuwa kama mavuno yaliyo kondeni. Wakati huo ndio uliokuwa wakati kwa Yesu kukusanya mavuno.

Chora duara kuzunguka matita ya ngano ambayo yako mbele ya sentensi yaliyo ya kweli.



Yesu aliwatuma wasaidizi sabini kutembelea miji na vijiji.



Aliwatuma wasaidizi hao wake katika kundi la watu watatu watatu.



Yesu aliwambia wasaidizi wake waombe ili kwamba watenda kazi wengine wengi waweze kutumwa.



Wasaidizi hawa sabini walishiriki Habari Njema na watu vijijini na mijini.

Yesu aliwapa wasaidizi wake maagizo au maongozi muhimu. Andika namba ya maneno yaliyo hapo chini ili kukamilisha maagizo hayo ambayo Yesu aliwapa wasaidizi wake.

1. Msichukue
2. Mnapingia nyumbani semeni
3. Mktanapo na watu njiani

3. msitumie wakati mwingi mkiamkuna.

1 fedha wala vifaa.

2 "Amani iwemo nyumbani humu!"



KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

Akawaambia, "Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache; basi mwombeni Bwana wa mavuno apeeke watenda kazi katika mavuno yake." Luka 10:2

Jambo linahitajika zaidi mno ni watenda kazi wa Kristo. Kuna watu ulimwenguni mwote wanaohitaji kuambiwa ahadi za ajabu za Yesu. Mamilioni ya watu hawajasikia kamwe Neno la Mungu, na mamilioni hawajapata kufahamu Mungu wa kweli anayeshi milele. Hata katika nchi yako na kijijini mwako, kuna watu unaowajua kwamba hawamfahamu Kristo kuwa Mwokozi wao.

Yesu aliwachagua wanafunzi sabini ili kuwatuma mijini na vijijini kueneza Injili ya wokovu. Watu hawa walikuwa wafuasi wa Bwana. Je, na sisi pia tu wafuasi? Bwana ametutuma kushiriki habari hii yake na watu wa ulimwengu. Kuna kazi nyingi ya kufanya lakini watenda kazi ni wachache. Je, wanaruhusu Mungu kukutumia katika kushiriki Habari Njema na wengine? (Mwalimu aweza kutumia munda fulani katika kuzungumza jinsi Mungu anavyotumia vijana katika kazi yake. Tilia mkazo ukweli kwamba wengine hujifunza kutoka kwa matendo yetu na nia zetu zaidi kuiko maneno yetu.)

KULIFUNGA SOMO

Njeri alielewa katika nyumba ambayo Mungu hakufahamu. Alikuwa amewasikia wazazi wake wakizungumza juu ya Yule anayelea mvua na radi na anayekaa mbali. Wazazi wake walikwisha kusema kwamba wanadamu hawawezi kumjua huyu Mungu; walakini, mara nyingi, Njeri alifikiria kwamba pengine Mungu aweza kujulikana.

KULIFUNDISHA SOMO

Po pote alipokwenda Yesu makutano ya watu walimfuata. Baadhi ya watu hawa walimwamini na kuyamini maneno aliyosema. Wengine walimstaajabia, wkamfuata kwa sababu walitaka kuona miujiza yake. Wengine hawakumwamini bali walimsikiliza tu wakitaka kumkamata kwa kosa lo lote ambalo angefanya, lakini hawakumpata na hatia yo yote.

Katika Luka 15:1-3, twasoma juu ya watu hawa. Watoza ushuru na wenye dhambi walihesabiwa kuwa watu wabaya lakini wengine kati yao walimpenda Yesu.

Yesu ndiye aliyekuwa mwalimu wa pekee ambaye alikuwa na moyo wakuwapenda. Aliwahurumia na kutaka wamjue na kumpenda Mungu.

Mafarisayo na waadishi walikuwa waangalifu sana katika kutii sheria za Mungu na sheria nyingine ambazo zilitungwa na viongozi wa kidini katika miaka mingi iliyopita.

Walijisifu kwa kusema, "Sisi ndio watu wema wa Mungu. Tunaepukana na dhambi. Hatufanyi urafiki na wenye dhambi. Hatui kamwe chakula kilichopikwa na wenye dhambi. Kwa kweli, Mungu anapendeza nasi."

Wayahudi walioiti sheria walipendeza na malundisho ya Yesu, lakini hawakuweza kuelewa jinsi alikuwa mtakaifu, na mii sheria, na hali alikula pamoja na wenye dhambi. Yesu aliwasilimia hadithi tatu kuwaonesha fikira zake juu ya watu wenye kupotea katika dhambi.

1. (Luka 15:3-7) oma hadithi hii katika Biblia. Pengine wanafunzi wako watapenda kuiga hadithi hii. Mwanbie mwanafunzi mmoja awe mwana-kondoo aliyepotea, na mwingine awe mchungaji anayekwenda kumtafuta. Wanafunzi wengine wawe jirani wanaofurahi wakati mwana-kondoo anapokatana.



2. (Luka 15:8-10) Hadithi hii pia inaweza kuigwa na wanafunzi. Katika hadithi hizi mbili, ni nani au kitu gani kinachosimama badala ya mwenye

dhambi? Ndiyo, ni mwana-kondoo na shilingi ile iliyopotea. Nani aliyesimama badala ya Mwokozi? Ndiyo, ni mchungaji na yule mwanamke.

Wote wawili walishughulika juu ya vitu vyao walivyopotea. Walifanya bidii kuvitafuta na kupipata tena. Yesu alikuja ulimwenguni kutafuta na kuwaokoa wenye kupotea dhambi.

3. Hadithi hii ni juu ya mwana mmoja ambaye pengine alikuwa umri sawa na wa mwanafunzi wa shule ya sekondari. Alijua kwamba siku fulani baba yake atagawa mali yake kati yake na nduguye mkubwa. Pengine alikuwa akifikiri kuwa maisha pale nyumbani kwao shambani hayajakuwa ya kupendeza. Siku moja alimwambia baba yake, "Nipe sehemu ya mali inayonianguka." Wadhani kwamba

YESU AELEZA JUU YA KUTAFUTA KILICHOPOTEA

MASOMO YA BIBLIA: Luka 15 KUJIANDAA KUFUNDISHA

Somo letu siku hii latuonyesha kwamba tumepaswa kuwa na upendo kwa wenye kupotea katika dhambi. Kuwashughulikia watu waliopotea dhambiini kunapaswa kuwa sehemu muhimu sana ya maisha ya Kikristo.

Waonaje juu ya upendo wako kwa Wakristo wengine? Hii pia ni muhimu.

Angalia unapoishi katika ulimwengu huu wako. Angalia darasa lako la Biblia. Pengine kuna mifoto darasani mwako mwenye kelele na unayemwona kuwa si mwenye adabu. Azungumza zaidi, na kuwasumbua wengine darasani, yaani asumbua darasa nzima. Je, wamfikiria nini? Je, watamani wakati mwingine ya kwamba asiwepo darasani, au asije tena? Tujiulize sisi wenyewe, "Je, naonyesha upendo kwa wenzangu?"

Watoto wadogo wanahitaji utunzi na upendo wetu. Wewe kama mwalimu wao, una nafasi ya kuona kwamba wanakua katika hali nzuri kwa sababu ya upendo. Tambua hitaji lao na uwe tayari kuwaonyesha kwamba unawashughulikia.

Itakuwa vigumu kuwafundisha wanafunzi hawa somo juu ya kuwapenda wenye dhambi ambao hawamjui Yesu ikiwa sisi wenyewe hatuwapendi watoto wa Mungu.

Siku moja alikutana na Wairimu kutoka kijiji jirani. Alikuwa hajamwona Wairimu kwa muda mrefu. Walipozungumza pamoja, Njeri alitambua kwamba Wairimu alikuwa na furaha sana. "Mbona unafurahi sana?" Njeri alimwuliza.

Wairimu alimjibu, akasema, "Juziuzi nilisikia habari za Mtu fulani anayenipenda na anayejua shida zangu. Zamani za kale mtu uyo alikuja kukaa ulimwenguni ili kwamba mimi pamoja nawengine tuweze kuwa na maisha mapya. Nimejifunza juu yake katika Biblia. Jina lake ni Yesu. Yeye ni Mwana wa Mungu. Naamini ya kwamba yu hai, na kwamba aweza kuyageuza maisha yangu. Nimejifunza kuzungumza na Mungu kwa maombi, na furaha kuu imekwisha kunijia maishani mwangu."

Ilikuwa vigumu kwa Njeri kuamini ya kwamba mtu ye yote aweza kupata furaha kuu katika jambo ambalo lilionekana kwake kuwa rahisi sana na lisilo na maana. Walakini, furaha ya msichana huyu ilikuwa halisi.

Njeri alijua kwamba alihitaji kuwa na furahakama hii. Alizungumza na Wairimu kwa muda mrefu sana. Walikutana pamoja kwa wiki kadha na kusoma Biblia. Baada ya muda kidogo, Njeri alitambua kwamba kuna Mungu anayempenda na kumlinda.

Njeri aliweza kumjua Kristo kwa sababu ya Wairimu aliyekuwa na furaha sana kwa kumjua Yesu na kutaka kushiriki naye Habari hii Njema. Je, ulimwengu huu si ungekuwa tofauti kama kila Mkristo angekuwa na furaha kama hiyo aliyokuwa nayo Wairimu?

Daudi aliandika zaburi yake, "Unirudishie furaha ya wokovu wako; unitegemeze kwa roho ya wepesi. Nitawafundisha wakosaji njia zako, na wenye dhambi watarejea kwako. (Zaburi 51:12-13)

Unapofunga kwa maombi, utahitaji kufanya kifungu hiki kutoka Zaburi kiwe tamaa ya maisha yako.

YESU AONYESHA NI NANI JIRANI MWEMA

MASOMO YA BIBLIA: Luka 10:25-37

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Masomo yaliyomo kitabuni humu yanaonyesha dhahiri mahitaji ya kumpa Kristo nafasi ya kwanza maishani mwetu. Kila somo linashughulika na njia fulani ambayo kwayo twaweza kumtukuza Kristo. Jaribu wki hii kuwasaidia wanafunzi wako kuona jinsi wanaweza kumpa Kristo nafasi ya kwanza kwa kuwapenda na kuwasaidia wengine. Wafanye wanafunzi wako wafahamu kwamba wanaonyesha upendo wa Kristo wakati wanapowapenda wengine.

Mwana-sheria anayesimuliwa katika somo la wki alijua kwamba ilimpasa kumpenda jirani yake, lakini hakuwa anafanya hivyo. Na katika njia hiyo, wawilana na wasichana wanaoifahamu hadithi hii ya Msamaria Mwema, wanaajua kwamba wanapaswa kuwapenda jirani zao. Yatupasa kuwasaidia kufanya hivyo. Omba ili kwamba Roho Mkatifu akusaidie kuwaonyesha wanafunzi wako jinsi wanavyoweza kumweka Kristo kwanza maishani mwao kwa kuwapenda na kuwasaidia wengine.

Kwa kupata maelezo zaidi, soma Kukumbuku la Torati 6:5 na Mambo ya Walawi 19:18. Vifungu hivi vinatupa msingi wa fundisho ambalo Yesu alimfundisha mwana-sheria. Labda utapenda kuonyesha kwamba amri

isemayo, "Mpende jirani yako kama nafsi yako" inatumika mara kwa mara katika Agano Jipya. Tumia vifungu viluatavyo kuonyesha umuhimu wa somo hili la leo: Warumi 13:9; Wagalatia 5:14; na Yakobo 2:8.

Labda utataka kutumia hadithi ya mwanafunzi mmoja mvulana au msichana mwenye umri sawa na wa wanafunzi wako, vile alivyoonyesha upendo kwa jirani yake. Pengine wanafahamu kijana mmoja aliyekoa maisha ya mwenzake. Hadithi kama hiyo itakuwa yenye kupendeza sana.

Unapofundisha, usisahau kusudi la somo hili: kufundisha ya kwamba jirani wema ni wale wanaompenda Bwana na kuonyesha upendo huo kwa kuwasaidia wengine.

MAMBO YA KUKAZA

1. Mungu atuumuru kumpenda, na pia kumpenda jirani yetu.
2. Hadithi ya Yesu ilionyesha kwamba jirani ni wale wanaohitaji msada wetu.
3. Jirani mwema humsaidia ye yote mwenye mahitaji, wala siyo rafiki yake peke yake.

KULIFUNDISHA SOMO

Sema: Hebu siku ya leo tukutane na mwana-sheria yule aliyesema na Yesu. Alikuwa mwana-sheria mwenye akili ambaye alijua sheria ya Agano la Kale. Alikata shauri kumwuliza Yesu swali akitaka kujua kama Yesu

mali tu ambayo tunaweza kuwa nayo leo na kesho?"

Mara kwa mara twafikiri ya kwamba vitu muhimu mno maishani ni kupata fedha ningi au nguo au kazi nzuri au kupata vitu ambavyo ni vya watu wengine. Akili zetu zikiwa zinashughulika na kufikiria vitu hivyo, tunakuwa na wakati mchache wa kufikiria upendo wa Mungu kwetu na vile tunavyoweza kuonyesha upendo huo kwa watu wengine.

Yatupasa kutumia nafasi zaidi kwa kusudi la kuwatumikia wengine. Yesu alitwambia ya kwamba vitu tunayowafanyia wengine vitakuwa kama hazina tunazowekewa mbinguni. Itakuwa jambo la huzuni kama tukitumia wakati wetu wote hapa ulimwenguni tukijitendea mambo ya kutupendeza sisi wenyewe.

KULIFUNGA SOMO

Watoto wahitaji kukumbushwa mambo ambayo wanaweza kuwafanyia wengine. Ingawa nafasi zipo kila siku, vijana wadogo mara nyingi hawawezi kutambua nafasi hizo.

Pengine waweza kuwakumbusha wanafunzi ya kwamba wanaweza kuwasaidia wengine katika jina la Yesu kwa kuwafanyia mambo yafuatayo:

Kutoa fedha zao kanisani kwa matumizi ya Yesu.

Kuwasaidia mama zao kwa kazi ya nyumbani.

Kusaidia kumlinga ndugu au dada yao.

Kuonyesha wema wao kwa mtu wao asiyePENDWA na mtu ye yote.

Na wewe, Mwalimu, labda waweza kufikiria mambo mengine.

Unapofunga somo hili kwa maombi, omba msada wa Mungu ili sisi sote tutumie wakati wetu tukifanya mambo yale yanayodumu kuiliko kutumia wakati wetu wote katika kujitafutia vitu ambavyo havinadumu.

La, akini Yesu alikuwa akisema ya kwamba hazina ya ulimwengu isiwe ya umuhimu sana kwetu kuliko ya mbinguni. Hii ni kwa sababu hazina ya mbinguni itadumu hata milele.

Uliza! Hazina yangu ya mbinguni ni nini?

Ni fedha, wakati, na nguvu zangu ninazotupia kwa ajili ya Kristo. Naweza kumweka Kristo kwanza maishani mwangu kwa njia ninayotumikia kila siku na kwa njia ambayo nawatumikia watu wengine katika jina lako.

KAZI YA KUFANYA

Mtu mmoja alitaka sehemu ya urithi wake kwa tamaa zaidi kuliko vile alivyotaka upendo wake Mungu. Yesu alimwambia kwamba alikuwa akitenda dhambi. Piga mstari chini ya neno la dhambi ambalo Yesu alimwonya mtu huyu kwalo.

Kuua Kudanganya Choyo Chuki

Mkulima yule tajiri pia alikuwa mtu mchoyo. Weka alama hii (X) katika nafasi zilizo kando ya sentensi zilizo kweli.

— Mavuno ya mkulima yule tajiri yalikuwa machache.


X_ Mkulima yule tajiri alikata shauri kujenga ghala kubwa zaidi.

— Alifikiri kwamba atakuwa maskini maishani mwake mwote.

X_ Mkulima yule tajiri alitaka kuishi maisha ya raha.

X_ Mungu aliondoa uhai wa mkulima yule tajiri kabla hajajenga ghala mpya.

Yesu alitumia mafunzo juu ya ndege ili kuwafundisha wafuasi wake somo. Chora mstari kutoka kwa picha ya ndege huyo hadi kwa maneno aliyoyasema Yesu.



Ikiwa Mungu anawalisha ndege hata sisi pia atatunza.

Yesu alisema kwamba kuwa na wasiwasi ni kubaya. Watu huwa na wasiwasi juu ya mambo mengi. Je, siku hizi watu huwa na wasiwasi juu ya mambo gani?

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Kwa kuwa hazina yenu ilipo, ndipo itakapokuwapo mloyo yenu." Luka 12:34

Labda inatupasa kunyamaza na kujiuliza, "Je, ni jambo lipi la muhimu mno maishani mwetu? Ni kitu kama

alijua sheria au la. Tena swali hilo alilouliza lilikuwa la kumtega Yesu atoe jibu lisilokubaliana na Maandiko ya Agano la Kale.

(Mwambie mwanafunzi mmoja ajifanye mwana-sheria. Asome maneno aliyosema mwana-sheria ambayo yanapatikana katika Luka 10:25,27, na 29. Mwambie mwana-funzi mwingine asome maneno ya Yesu katika Luka 10:26 na 28.)

Uliza: Je, wafikiri ya kwamba yule mwana-sheria alitaka kujifunza kweli juu ya maisha ya milele? Je, Yesu alipumbazwa na swali hilo la kumtega?

Yesu alimjibu mwana-sheria kwa kumwuliza swali. Akamwuliza, "Umekwisha jifunza sheria wewe mwenyewe na unaweza kujibu swali lako. Imeandikwa nini katika torati juu ya kuwa na uzima wa milele?"

Jibu la mwana-sheria ndicho kifungu tunachotaka kukumbuka leo.

(Wakati huu ndio unaofaa sana katika somo kufundisha kifungu cha kukumbuka.)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako." Luka 10:27

Je, mwamfahamu ye yote ambaye amefanya mambo haya yote tunayofundishwa na kifungu hiki? La, sisi sote tumekwisha kuvunja amri hii, na yule mwana-sheria pia alikwisha kuvunja.

Kwa upesi yule mwana-sheria aliuza swali lingine. "Ni nani jirani yangu?" Yesu alisimulia hadithi ifuatayo kumsaidia aelewe hasa ni nani aliyekuwa jirani yake. (Soma Luka 10:30-35.) Hii ndiyo hadithi tunayojua kwa jina la "Msamaria Mwema."

Njia itokayo Yerusalemu kwenda Yeriko ilikuwa ya mteremko zaidi. Ilikuwa na mapango mengi na miamba ambayo wanyang'anyi na wahalifu wengine walijificha. Je, barabara kama hiyo ni salama kwa mtu kusafiria peke yake? La, na watu wote wa sehemu hiyo walijua hivyo.

Katika hadithi hii tunayosoma kutoka Biblia ni jambo gani lililomfanyikia yule mtu? Alikuwa amenyang'anywa, na kupigwa, na kuachwa njiani akiwa karibu kufa. Alipokuwa pale njiani, pengine aliomba moyoni kwamba mtu apatie pale na kumsaidia. Mara alisikia vishindo vya nyayo ya mtu akija. Alikuwa na shukrani nyingi. Alipoweza kumwona mtu huyo ajaye, alifurahi mno. Aliweza kumtambua kwa joho alilovaa kuwa ni kuhani. "Kwa kweli, kuhani wa hekalu la Mungu atanisaidia," alifikiri.

Lakini kuhani huyo alimwagaia na hakusimama ili kumsaidia. Hata alipitia kando ya njia ili kuepukana naye.

Baada ya muda kidogo, mtu mwingine alikuja. Mtu huyo alikuwa Mlawi, mtu aliyetumikia katika ibada za hekalu. Pengine angemsaidia. Lakini la, hakumsaidia. Mlawi huyo

alimtaazama tu na akapia kando ya njia.

Labda watu hawa waliogopa wakifikiri kwamba wanyang'anyi walikuwa wanguai karibu. Labda walikuwa na haraka kwa sababu fulani. Kwa kwele, wakati huu yule majeruhi alikuwa na huzuni zaidi na kujisikia katika hali ya upweke mno. Alikuwa hana fedha, nguo, na alikuwa akiokwa na damu na kutojiweza. Je, kuna mtu aliyenajali? Kuna mtu aliyemsaidia? Je, aliachwa hapo njiani kufa?

Baada ya muda kidogo alimsikia msafiri mwingine akija. abda wakati huu alikuwa amekwisha kufa moyo kwamba hakuna mtu atakayemsaidia.

Msafiri huyu aliyekuwa akija alikuwa Msamaria. Wayahudi hawakushirikiana na Wasamaria. Wayahudi wengine walianini kwamba Mungu hakuwapenda Wasamaria. Kwa kwele, huyu majeruhi hakumtaazama Msamaria huyo kumsaidia. Lakini je, kufanyika nini? Msamaria hakusimama tu na kumfunga jeraha zake, bali alimwinua na kumweka juu ya punda wake na kumpeleka katika nyumba ya wageni ambako angetunzwa mpaka angekuwa mzima tena. Msamaria huyo alimlipa mwenye nyumba ya wageni fedha za utunzi wake kwa Myahudi huyo aliyejeruhiwa.

Uliza: Ni nani aliyekuwa jirani mwema? Ndiyo, yule Msamaria ndiye aliyekuwa jirani mwema.

Hadithi iliipokwisha, Yesu alimtaazama yule mwana-sheria,

akamwuliza swali. "Waonaje kati ya hao watatu, ni yupi aliyekuwa jirani mwema?" Mwana-sheria alijua jibu kwa mara moja. Yesu alitaka kumwonyesha kwamba jirani mwema ni yule anayeonyesha upendo na huruma kwa mtu ye yote mwenye mahitaji. Kuwa jirani mwema hakutegemei mahali mtu anapokaa. Mtu anaweza kuwa wa kabila letu au lingine. Jirani mwema aweza kuwa rafiki au adui.

Uliza: Kama ukimwuliza Yesu kwamba ni yupi jirani yako wafikiri atasema nini?

Uliza: Waweza kumfikiria mtu unayeweza kumsaidia?

Na rafiki zako, ndugu au dada yako, mama au baba yako, na mwalimu wako, je? Na mwalana au msichana wa kabila lingine anayesoma shuleni mweni ambaye yu katika hali ya upweke, je? Mungu atakusaidia kuwa jirani mwema kama utamwomba.

Wiki hii, hebu tufanye juhudi maalumu ili tuwe majirani wema wa mtu fulani anayehitaji rafiki. Na tukumbuke kitando hicho chema ili tuweze kushirikiana kwalo na wanafunzi wa darasa siku ya somo lijalo.

KAZI YA KUFANYA

Labda utapenda kuzunguka darasani kuwasaidia wanafunzi kuandika majibu sawa ya maswali na kuhakikisha kwamba wanafanya kazi sawasawa. Labda utataka kukaza sehemu fulani ya somo hili wakati

mkulima mpumbavu. Hatujawa tajiri na kumsahau Mungu. Kwani tuliacha kazi zetu ili kumtumikia Yesu."

Lakini, Yesu alijua kwamba wanafunzi hawa wanaweza kujaribiwa kuwa na wasiwasi. Je, Mungu angewapa vitu waliyohitaji kwa kuishi? Kwa ajili hiyo Yesu aliwaambia, "Msisumbukie masha yenu, mtakula nini; wala miili yenu, mtavaa nini." Maagizo hayo ya Yesu kwao yanapatikana katika Luka 12:22-27. (Mwulize wanafunzi wako mmoja asome vifungu hivi kwa darasa.)

Yesu aliwaambia wanafunzi hawa wake wafikirie ndege wa angani ambao hawapandi wala hawalimi wala kuweka mavuno. Mungu ndiye anawalisha. Na ikiwa anawalinda ndege hawa, kwa kwele atawalisha pia watu wake ambao wana thamani kuu kwake kuliko ndege.

Yesu alitaka wafuasi wake wamwamini Mungu katika kuwalinda. Alitaka waelewe kwamba kuwa na wasiwasi hakuna maana na pia ni dhambi. Kwa hivyo, aliwauliza swali katika kifungu cha 25. Alikuwa akiuliza kama kuna ye yote anayeweza kujiongeza uhai wake kwa kuwa na wasiwasi. Wanafunzi walijua hakuna ye yote ambaye aliweza kujiongeza uhai wake. Kisha Yesu aliuuliza, "Basi, ikiwa hamwezi hata neno lililo dogo kwa nini kujisumbua kwa ajili ya yale mengine?" Alitaja maua yanayomea makondeni. Hayatendi kazi, lakini Mungu anayavika. Kwa kwele, Mungu atawapa watoto wake mahitaji yao.

Wakristo wanapaswa kufanya nini badala ya kuwa na wasiwasi na kuwa wachoyo? Yesu alitaka wafuasi wake kupendelewa zaidi kuwa wake na kuwasaidia wengine kuliko kitu cho chote. Bwana Yesu ataka leo tupendewe zaidi na kazi yake kuliko kitu kingine cho chote. Tukifanya hivi tunapokea ahadi yake kwamba tutapata kitu cho chote tunachohitaji.

Kutokana na somo hili kwaweza kuona ya kwamba natupasa kuchagua mahali pa kuweka hazina yetu, kama ni ulimwengu au mbinguni. Je, Yesu alisema jambo gani katika Luka 12:34 ambalo linaeleza mahali hazina yetu ipo? Kifungu hiki maana yake ni kwamba mahali ambapo fikira yako ipo, na ambapo kazi yako ipo, nipo kitu unachothamani zaidi kipo.

Fikiria hazina ya ulimwengu ambayo unatamani kuwa nayo. Labda ni baiskeli. Kama ukiwa na baiskeli mpya, utaitunza na kukaa nayo kwa muda gani? Labda utaitunza kwa miaka michache, au kwa muda mrefu mpaka utakapokufa. Kisha baiskeli hiyo itakuwa ya mtu mwingine. Lakini tunapomfanya mtu fulani kitu katika jina la Yesu tunaweza hazina yetu mbinguni, na itakuwa yetu hata milele. Hakuna anayeweza kutunyang'anya wala haitaharibika kwa ajili ya kukaa sana.

Je, Yesu alikuwa akisema hapa ya kwamba tusiwe watu wa furaha wala kuvitunza vitu anayotupa? Lai Je, ni vibaya kutaka baiskeli? (Wape wanafunzi wako wakati waku-zungumza juu ya jambo hili.)

"Bwata, mwambie ndugu yangu angavie mali ambayo baba yetu alituaia."

Yesu alimwambia mtu huyu ya kwamba kazi yake haikuwa ya kuanua ugomvi kati ya jamaa. Walakini, alidhihirisha kina cha shida aliyokuwa nayo. Jambo ambalo lilikuwa chanzo cha shida ya mtu huyu lilikuwa ni tamaa au choyo. Yesu alimwambia, "Jilindeni na choyo."

Uliza: Na hii maana yake nini?

(Wape muda wanafunzi wako wazungumze juu ya swali hili; na kutoa jibu.)

"Choyo" ni kutamani kuwa na vitu vingi zaidi ambavyo watu wanavyo hapa ulimwenguni. Mtu mchoyo hufikiri ati vitu hivi ni vya muhimu kwa furaha. Hata hutamani vitu vya wengine kuwa vyake.

Uliza: Kwa nini choyo ni dhambi? Yesu aliwasilimulia watu hadiithi ili kuwawezesha wapate kuelewa.

(Mwambie mwanafunzi wako mmoja asome Luka 12:16-21.)

Hapo kale palikuwako mkulima mmoja tajiri ambaye shamba lake lilizaa mavuno mengi ambayo hayakuweza kuweka yote katika ghala zake. Basi, alikata shauri kuvunja ghala zake na kujenga nyingine



kubwa. Na baada ya kuweka mavuno yake yote katika ghala hizo mpya, alipanga kujiambia, "Ee nafsi yangu, una vitu vingi ulivyojwekea akiba kwa miaka mingi. Pumzika. Kula, kunywa na ufurahi."

Wakati ule tajiri alipofanya mipango hii, alimsikia Bwana Mungu akisema naye. Bwana alimwambia, "Mpumbavu wewe, usiku huu wa leo wanataka roho yako! Na vitu ulivyojwekea tayari vitakuwa vya nani?"

Mkulima yule tajiri alifikiri kwamba alikuwa na vitu vyote alivyohitaji maishani na kwamba kwa miaka mingi ataweza kukaa kwa raha bila kufanya kazi yo yote. Lakini alikuwa amesahau kitu kimoja muhimu. Ingawa alikuwa tajiri, hakuweza kuongeza miaka ya maisha yake. Fedha zake hazikuweza kumsaidia hata kidogo wakati kifo chake kilipomjia. Alikuwa amefikiria tu ghala ZAKE, mavuno YAKE, na mali YAKE. Je, aliweza kuchukua kimoja kati ya vitu hivi wakati alipokufa? La. Kwa hivyo, kwa kweli alikuwa mtu maskini sana.

Yesu alikuwa akifundisha kwamba kila mtu anayekaa katika maisha ya choyo akijiwekea mali ni mtu maskini kama yule tajiri mpumbavu alivyokuwa. Watu wa pekee ambao ni tajiri kweli ni wale ambao "wanaweka hazina zao mbinguni" kwa kumweka Kristo kwanza maishani mwao na kuwatumikia wengine katika jina lake.

Wanafunzi wa Yesu walikwisha kumsikiliza kwa uangalifu. Pengine walikuwa wakifikiri, "Sisi si kama yule

unapowasaidia wanafunzi kwa kazi yao.

Agano la Kale lilitoa amri fulani kwa watu kufuata. Chora mistari kutoka sehemu ya kwanza ya amri hizo hadi kwa maneno yote yanayokamilisha amri hizo.

Mpende Bwana Mungu wako kwa

moyo fedha roho rafiki nguvu akili

Mpende jirani yako kama wengine nafsi yako

Yesu alisimulia hadithi hii ili kuonyesha vile jirani mwema alivyo. Piga mstari chini ya maneno yaliyo kweli juu ya watu watatu wanaosimuliwa katika hadithi hii.

MTU FULANI

alishikwa na wanyang'anyi.
nguo zake ziliibwa.

alijeruhiwa.

alikuwa karibu ya kufa.

KUHANU

alimwona mtu huyo alivejeruhiwa.

alimpa huyo majeruhi nguo.

alipitia kando ya njia.

alimwombea majeruhi huyo.

MLAWI

alimtakwama majeruhi.

alipitia kando ya njia.

alimhurumia mjeruhi.

alimpiga teke.

Piga mstari chini ya maneno ya kumalizia ambayo ni muhimu.

Jirani Mwema

huwasaidia wengine ili nao wampende.

huwasaidia watu anaowapenda.

huwasaidia watu wenye mahitaji kwa sababu ampenda Yesu.

huwasaidia watu wenye mahitaji kwa sababu ataka ajisikie "vema".

Picha za hapo chini zaonyesha Msamaria Mwema akisaidia. Baada ya wewe kusoma vifungu vya Biblia, tazama picha hizo kwa uangalifu. Kando ya kila picha andika namba ya kifungu cha Biblia ambacho kinaeleza juu yake.



"Mtunze, nitakulipa." Kifungu cha 35.



"Alifunga majeraha ya yule majeruhi." Kifungu cha 34.



Yatupasa kufanya mambo hayo
mema kama matokeo ya upendo
wetu.

Labda utataka kuwaonyesha
wanafunzi wako mahitaji ya
kumpenda Mungu kwa mioyo yetu,
kwa roho zetu, kwa nguvu zetu, na
kwa akili zetu. Tukifanya hivyo
itakuwa rahisi kwetu kuwependa
njirani zetu.

Alimhurumia yule majeruhi."
Kifungu cha 33.

KUFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Mpende Bwana Mungu wako
kwa moyo wako wote, na kwa roho
yako yote, na kwa nguvu zako zote,
na kwa akili zako zote; na jirani
yako kama nafsi yako." Luka 10:27

Tunapotei amri na kumpenda
Mungu itakuwa rahisi kumpenda
jirani yetu. a ikiwa hatumpendi
Mungu kama inavyotupasa ni vigumu
kuwependa wengine. Kuwatendea
wengine mambo mema hakutoshi.

YESU AZUNGUMZA JUU YA HAZINA YA MBINGUNI

MASOMO YA BIBLIA: Luka
12:13-34

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Kukumbuka somo tulilojifunza
wiki jana juu ya jirani mwema
kunaweza kuwa njia ya kuanzisha
somo hili la leo. Na kwa vile
wanafunzi walilizwa kuwa majirani
wema kwa mtu fulani wiki hii,
hakikisha uwaambie waeleze mambo
walivyokwisha kufanya. Wanapoeleza
mambo walivyokwisha kuyaona, labda
waweza kuwauliza ikiwa ni rahisi
daima kuwa jirani mwema. Waweza
kuwaonyesha ya kwamba
tunapomsaidia bila kutarajia malipo,
hazina zetu tunaziweka mbinguni
kama tunavyofundishwa na somo hili
la leo. Jaribu kuwasaidia wanafunzi
kuona kwamba masomo haya mawili
yanafanana sana.

Chagua hadithi juu ya kijana
mmoja mdogo wa rika la wanafunzi
wako ambaye amekwisha kumfanya
mtu mwingine jambo bila kutazamia
malipo. Kunao wakati mwingi
maishani mwa wanafunzi ambapo
nafasi ya kusaidia ipo. Waweza
kuwasaidia kuona kwamba
hatuwasaidii wengine ili tuweze
kulipwa, bali kuna furaha
tunayopokea wakati tunapokuwa
watu wenye kusaidia.

Mara nyingi Yesu alieleza juu ya
watu ambao walitumia wakati wao
wote na nguvu zao kupata vitu vya
kutumia hapa ulimwenguni. Aliitaka

kutonyesha kwamba vitu hivyo si vya
muhimu kama vile vinavyodumu
milele. Yesu alivita vitu vinavyodumu
milele kuwa ni "hazina ya mbinguni."
Wiki hii tutajifunza hadithi mwingine
ya watu ambao walifikiri kwamba vitu
vya ulimwengu vilikuwa muhimu sana
kuliko vitu vya mbinguni. Kusudi la
somo hili ni kuwafundisha

wanafunzi ya kwamba tusiwe
wachoyo kwa kutafuta anasa
maishani mwetu, lakini ya tupasa
tuweke hazina yetu mbinguni.


MAMBO YA KUKAZA

1. Yesu alionya kwamba tusiwe
wachoyo au kutumia wakati
wetu wote tukitafuta anasa maishani
mwetu.

2. Mali na fedha huwa juu kama
tukivifanya kuwa vitu muhimu sana
maishani mwetu.

3. "Tajiri" hasa ni yule anayemweka
Kristo kwanza maishani mwake.

KULIFUNDISHA SOMO



Siku
moja, mtu
mmoja
mwenye
tamaa
alikuuwa
akimsikiliza
Yesu
akifundisha.

Aliikuwa na
shida ambayo alitumaini kwamba
Yesu angemsuluhisha. Alisema,